# MIKATABA YA UWEKEZAJI KATI YA NCHI MBILI (MIUMBI) NA ATHARI ZAKE KWA TANZANIA



The Agreement was previously published as Tanzania No. 1 (1994) Cm 2593

TANZANIA

Treaty Series No. 90 (1996)

Agreement

between the Government of the United Kingdom of Great Britain and Northern Ireland and the Government of the United Republic of Tanzania

for the Promotion and Protection of Investments

Agreement between

the Government of the Republic of Finland

and

the Government of the United Republic of Tanzania

on

the Promotion and Protection of Investments

The Government of the Republic of Finland and the Government of the United Republic of Tanzania, hereinafter referred to as the "Contracting Parties",

RECOGNISING the need to protect investments of the investors of one Contracting Party in the territory of the other Contracting Party on a non-discriminatory basis;

DESIRING to promote greater economic co-operation between them, with respect to investments by nationals and companies of one Contracting Party in the territory of the other Contracting Party;

RECOGNISING that agreement on the treatment to be accorded such investments will stimulate the flow of private capital and the economic development of the Contracting Parties;

STOP THE UNFAIR INVESTOR-STATE DISPUTE SETTLEMENT AGAINST AFRICA

*Civil Society and Trade Union Statement to oppose the recent World Bank Court ruling against Tanzania*

Mindful of the crucial role investment can play in promoting economic growth and development, we Civil Society groups and Trade Unions in the United Republic of Tanzania together with Civil Society Organizations and Global Union Federations of the various Regional Economic Communities of the African continent wish to register out concerns about the growing number of legal suits multinational companies have brought against the Tanzania government in particular and other African States in general.

## Tanzania Trade and Investment Coalition
## TATIC

# MIKATABA YA UWEKEZAJI KATI YA NCHI MBILI (MIUMBI) NA ATHARI ZAKE KWA TANZANIA

Tanzania Trade and Investment Coalition (TATIC)

Waandishi: Sabatho Nyamsenda & Amani Mhinda

Kimechapishwa na:
Tanzania Trade and Investment Coalition
195 Garden Avenue, Mikocheni
Dar es Salaam
Julai 2022

Kimesanifiwa na:
Rogers Mahanyu

Kimepigwa chapa na:
Raita Company Ltd

Mchapishaji wa kitabu hiki anatoa ruhusa kwa mtu au taasisi yoyote kurudufisha, kunukuu na kuchapisha kitabu hiki kwa matumizi ya kielimu.

# TABARUKU

kwa kumbukumbu ya Padri Privatus Karugendo

*Ipo siku itatimia. Ndiyo, itatimia, ile ndoto yako ya kuiona Afrika iliyo huru, inayojitegemea kiuchumi na yenye kuamua mustakabali wake na kutumia rasilimali zake kwa ustawi wa watu wake.*

# YALIYOMO

Shukurani ........................................................................ v

Dibaji ............................................................................... vi

Utangulizi ........................................................................ viii

Sura ya 1:
Mfumo wa Ubepari na Uibukaji wa Sheria na Mikataba ya Kimataifa ........................................................................ 1

Sura ya 2:
Mageuzi ya Soko Huria na Utitiri wa MIUMBI ........ 15

Sura ya 3:
Vipengele Mahususi vya MIUMBI .............................. 25

Sura ya 4:
Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji ............................. 39

Sura ya 5:
MIUMBI Iliyoingiwa na Tanzania na Athari Zake .... 51

# SHUKURANI

Kitabu hiki kisingeweza kukamilika bila msaada, ushauri na uwezeshaji wa watu na taasisi mbali mbali. Shukurani za dhati ziende kwa Taasisi ya Rosa Luxemburg – Ofisi ya Afrika Mashariki ambayo imekuwa ikitoa ufadhili ili kufanikisha shughuli za Tanzania Trade and Investment Coalition (TATIC) zinazohusu MIUMBI. Utafiti, uandishi, uchapishaji na usambazaji wa kitabu hiki ni sehemu ya ushirikiano huo.

Tunapenda pia kuwashukuru Dk. Ng'wanza Kamata wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wakili msomi Stephen Msechu ambao walipitia mswada wa awali wa kitabu hiki na kutoa maoni ambayo yalitumika kuuboresha. Maoni mengine yalitoka kwa Boniface Kamara, Olivia Costa na Dorothee Braun. Hussein Hamza na Daudi Edward walisaidia kusahihisha makosa ya chapa. Tunawashukuru sana.

Tunapenda kutoa shukurani zetu kwa taasisi ya Hakimadini pamoja na wanachama wengine wa TATIC ambao wamekuwa wakishiriki katika kuchambua mfumo wa kimataifa wa biashara na uwekezaji na kutafakari mbadala wake.

# DIBAJI

Tanzania Trade and Investment Coalition (TATIC) ni muunganiko wa asasi mbalimbali za kiraia zinazofanya kazi zake Tanzania Bara, wanazuoni, wanahabari na vyama vya wafanyakazi. TATIC ilianza kufanya kazi zake mwaka 2018, ikijihusisha na uchambuzi na uchechemuzi wa sera, sheria na mikataba inayohusu biashara na uwekezaji. Maono ya TATIC ni kuwa na taifa lenye ustawi na maendeleo shirikishi na yenye usawa kwa kizazi cha sasa na kijacho. TATIC inaamini kuwa Tanzania, kama nchi huru, inapaswa kuwa kumiliki na kuwa na mamlaka juu ya biashara na uwekezaji ili kuleta maendeleo ya haki na usawa kwa wananchi wake.

Katika miaka minne ya uwepo wake, TATIC imefanya uchambuzi wa mikataba mbalimbali ikiwemo Mkataba wa Kimataifa wa Nishati (*Energy Charter Treaty*), Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*African Continental Free Trade Area* – AfCFTA), Mwongozo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu MIUMBI (*EAC Model BIT*) pamoja na MIUMBI iliyosainiwa na Tanzania. TATIC imezitumia chambuzi hizo kutoa mafunzo na ushauri kwa wabunge, wizara na taasisi mbalimbali za serikali, ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kitabu hiki, kilichoandikwa na Sabatho Nyamsenda na Amani Mhinda, ni mwendelezo wa jitihada za TATIC kutoa elimu na ushauri juu ya masuala ya yanayohusiana na biashara na uwekezaji katika nchi yetu.  Nyamsenda ni mwanataaluma

na mwandishi wa vitabu na makala mbalimbali na Mhinda ni mwanasheria, mwanaharakati na mchambuzi mahiri. Wawili hawa wana uzoefu wa kufanya utafiti katika masuala ya siasa–uchumi na wamekuwa mstari wa mbele katika shughuli za TATIC tangu kuanzishwa kwake.

Kitabu hiki kinatoa uchambuzi wa siasa-uchumi kuhusu MIUMBI na athari zake kwa nchi ya dunia ya tatu kama Tanzania. Waandishi wametumia lugha rahisi ambayo msomaji yeyote anaweza kuielewa hata kama ni mara ya kwanza kusikia kuhusu MIUMBI. Ni jambo la kutia faraja kuwa kitabu hiki kimeandikwa kwa lugha yetu wenyewe. Msomaji atapata mifano dhahiri kuhusu mambo yaliyojiri kihistoria hadi kufikia nchi kuanza kuwekeana mikataba ya uwekezaji. Msomaji pia atajifunza kuhusu athari za MIUMBI kwa nchi maskini, zikiwemo kesi mbalimbali zilizofunguliwa na kampuni za uwekezaji na mifumo ya uendeshaji wa kesi hizi. Kitabu kimetoa mifano hai ya kesi zilizofunguliwa dhidi ya nchi yetu Tanzania na namna zinavyoigharimu.

Ni matumaini yetu kuwa kitabu hiki kitasaidia kukuza uelewa watu wa nyanja tofauti tofauti, kuanzia wanafunzi wa ngazi mbalimbali hadi wafanyakazi wa sekta na idara mbalimbali, juu ya MIUMBI na madhara yake kwa Tanzania.

Olivia Costa<br>
Mkurugenzi, TATIC<br>
Julai 16, 2022

# UTANGULIZI

Kitabu hiki kimeandikwa mahususi ili kitumike kama nyenzo ya kujielimisha kuhusu mikataba ya uwekezaji kati ya nchi mbili (MIUMBI). Kama ilivyofafanuliwa ndani ya kitabu hiki, MIUMBI ni mikataba inayosainiwa kati ya nchi mbili kwa lengo la kulinda na kuhamasisha uwekezaji unaofanywa na nchi mojawapo katika nchi ya pili. Mikataba hii imekuwa ikipigiwa chapuo na nchi za Magharibi, mashirika ya kimataifa kama Benki ya Dunia, Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF) na Shirika la Kimataifa la Biashara (WTO) kama njia pekee ya kuongeza uwekezaji katika nchi maskini na hivyo kupelekea kukua kwa uchumi na kupungua kwa umaskini katika nchi hizo. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka katika nchi zinazopokea uwekezaji kuwa mikataba hii imekuwa ikitumika kama nyenzo za kuendeleza unyonyaji na uporaji wa rasilimali za nchi maskini unaofanywa na nchi tajiri. Kwa kuwa nchi yetu, Tanzania, ni miongoni mwa nchi zilizosaini mikataba ya aina hiyo, basi itakuwa ni jambo jema kwa wananchi pamoja na watunga sera kujielimisha kuhusu chimbuko na asili ya mikataba hii pamoja na athari zake kwa nchi yetu.

Kitabu hiki kimegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza imetoa maana ya MIUMBI pamoja na kuangazia chimbuko lake. Kwa mujibu wa sura hii, MIUMBI inapaswa kutazamwa kwa miwani ya kihistoria kwani chimbuko lake lipo katika historia ya mfumo wa kidunia wa kibepari. Sura hii imefafanua maana ya ubepari na kuonyesha tabia zake pamoja na hatua

ulizopitia. Pia, sura hii imeonyesha athari za mfumo wa kidunia wa kibepari kwa bara la Afrika. Na ni katika tumbo la ubepari ndimo tukutamo mikataba na sheria za kimataifa ambazo ziliwekwa mahususi kwa ajili ya kulinda unyonyaji na uporaji uliokuwa ukifanywa na nchi za Magharibi kwa nchi maskini. Unyonyaji na uporaji uliochambuliwa katika sura ya kwanza umegusia zama mbili za ubepari wa kidunia kama ulivyojidhihirisha barani Afrika: zama za biashara ya utumwa zilizoanza karne ya 16 hadi katikati mwa karne ya 19 na zama za ukoloni mkongwe ulioanza katikati mwa karne ya 19 hadi katikati mwa karne ya 20.

Sura ya pili inauchambua ubepari wa kidunia katika sura ya ukoloni mamboleo ambao ulianza miaka ya 1960 baada ya Afrika kujinyakulia uhuru. Kama ambavyo sura hii imeonyesha, japokuwa nchi za Magharibi ziliendelea kuzinyonya nchi za Afrika kupitia ukoloni mamboleo, nchi za Afrika ziliungana na nchi za Asia na Amerika ya Kusini kwa minajili ya kudhibiti chumi zake na kutumia rasilimali za nchi hizo kwa manufaa ya wananchi. Ni katika kipindi hicho ndipo nchi hizo zilitumia uwingi wao katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na kufanikiwa kupitisha maazimio yaliyolenga kusimika mamlaka ya kudumu ya nchi za dunia ya tatu juu ya rasilimali zinazopatikana katika nchi hizo. Kwa kuchukua hatua hizo, nchi maskini ziliweza kupunguza makali ya unyonyaji uliokuwa ukifanywa na nchi za Magharibi. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1980, nchi za Magharibi zilianza kurejesha upya makali ya unyonyaji na uporaji wao kwa nchi maskini huku zikitumia vyombo vya kimataifa kama Benki ya

Dunia, Shirika la Kimataifa la Fedha na Shirika la Kimataifa la Biashara kulazimisha nchi maskini kutekeleza masharti ya kulegeza uchumi.  Ni katika kipindi hicho pia ndipo idadi ya MIUMBI kati ya nchi za Magharibi na nchi za dunia ya tatu iliongezeka kwa kasi kubwa ikiwa na lengo la kulinda haki ya nchi tajiri kuzinyonya nchi maskini.

Sura ya tatu imefafanua vipengele vikuu vya MIUMBI na kuonyesha athari zake kwa nchi za dunia ya tatu. Sura hii imeonyesha kuwa MIUMBI huruhusu wawekezaji kuhamisha mitaji na faida kurejesha katika nchi zao na pia huwapa wawekezaji toka nchi iliyosaini MIUMBI upendeleo sawa na wawekezaji wa ndani au wawekezaji wa nchi nyingine yoyote iliyopewa unafuu wa kibiashara. Kadhalika, wawekezaji hupewa vibali vya kazi kwa ajili ya wafanyakazi wageni na hulindwa ili mali zao zisitaifishwe moja kwa moja au kwa kupitia mlango wa nyuma.  Hata baada ya nchi kujiondoa katika MIUMBI, bado mkataba husika huendelea kulinda uwekezaji kutoka nchi ya pili kwa miaka 10 au 15. Athari zake ni nyingi kwa nchi za dunia ya tatu, zikiwemo kupungua kwa uhuru wa nchi kujiamulia mambo yake yenyewe, kupoteza nafasi ya kulinda wawekezaji wa ndani na kutokuwa na nguvu ya kudhibiti utoroshaji wa mtaji na uporaji wa rasilimali zake.

Bila shaka kipengele cha MIUMBI kilichopigiwa kelele zaidi ni kile kinachoruhusu wawekezaji kuiburuza nchi walimowekeza katika mahakama za kimataifa. Kipengele hiki kimefafanuliwa kwa kina katika sura ya nne, ambayo imebainisha mifumo mbalimbali ya kimataifa ya usuluhishi wa migogoro ya

kiuwekezaji, ikaonyesha changamoto zake na kutoa mbadala. Sura hii haijamung'unya maneno katika kuweka wazi kuwa mifumo ya kimataifa ya utatuzi wa migogoro ilianzishwa kwa ajili ya kulinda maslahi ya wawekezaji kutoka ughaibuni.

Sura ya tano imeainisha MIUMBI iliyosainiwa na Tanzania, na kuorodhesha kesi zilizofunguliwa katika Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID) kwa kutumia mwanya uliotolewa kwenye MIUMBI na kuonyesha namna nchi inavyokamuliwa na kampuni kutoka ughaibuni pale zinapopeleka mashitaka yao katika vyombo vya utatuzi wa migogoro vya kimataifa. Katika hitimisho, sura hii imetoa ushauri kwa Tanzania kujiondoa kwenye MIUMBI yote pamoja na vyombo vya kimataifa vya usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji.

Katika sura ya tano pia limetolewa pendekezo kwa Tanzania kufanya mageuzi katika sheria zake, ikiwemo Katiba – ambayo ndiyo sheria mama – ili kusimika mamlaka ya kudumu ya Tanzania kujiamulia mambo yake yenyewe na kuondoa mwanya wa kampuni kutoka ughaibuni kuishitaki Tanzania kupitia vyombo vya kimataifa vya usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji.

Pengine zitaibuka hofu kuwa iwapo zitatekelezwa, hatua zilizopendekezwa katika sura ya tano zitawakimbiza wawekezaji! Hofu hizi, kama ambavyo inaonyeshwa katika sura hiyo, hazina msingi wa kisayansi kwani nchi kadhaa zimeshachukua hatua kama hizo na uwekezaji uliendelea

kuongezeka badala ya kupungua.

Katika miaka ya 1960 na 1970, Tanzania ilikuwa mstari wa mbele katika kupigania usawa katika mfumo wa kimataifa wa kiuchumi pamoja na haki na mamlaka ya kudumu ya nchi za dunia ya tatu juu ya utajiri asilia na rasilimali zake. Ni wakati sasa wa Tanzania kurudi katika misingi hiyo kwa kujiunga na vuguvugu la kuondoa unyonyaji na uporaji unaofanywa na nchi tajiri kwa nchi maskini unaolindwa na MIUMBI. Ni matumaini yetu kuwa kitabu hiki kitasaidia katika safari ya kurejea katika misingi hiyo.

Sabatho Nyamsenda & Amani Mhinda
Dar es Salaam & Nairobi
Julai 16, 2022

# SURA YA KWANZA

# MFUMO WA UBEPARI NA UIBUKAJI WA SHERIA NA MIKATABA YA KIMATAIFA

**MIUMBI ni nini?**

Mikataba ya Uwekezaji kati ya Nchi Mbili (MIUMBI), ambayo hujulikana kwa Kiingereza kama *Bilateral Investment Treaties* (BITs), ni mikataba inayosainiwa na nchi mbili kwa lengo la kulinda maslahi na mitaji ya wawekezaji wa nchi moja ndani ya nchi ya pili. MIUMBI ina vipengele kadhaa, tangu vile vinavyozuia utaifishaji wa mitaji ya wawekezaji hadi vile vinavyozipa mamlaka kampuni za uwekezaji kuiburuza nchi zilimowekeza katika mahakama za kibiashara za kimataifa. Vipengele vya msingi katika MIUMBI vimejadiliwa katika sura ya 3 ya kitabu hiki na athari zake kwa nchi maskini zimefafanuliwa.

MIUMBI husainiwa na nchi mbalimbali lakini sehemu kubwa ya MIUMBI imesainiwa baina ya nchi tajiri kama Uingereza na nchi maskini kama Tanzania. Hii ni kusema kuwa MIUMBI husainiwa baina ya nchi zisizo na usawa wa kiuchumi. Tofauti

hizi za nguvu za kiuchumi siyo za asili bali ni matokeo ya mahusiano ya kinyonyaji baina yao, yanayozifaidisha nchi tajiri na kuzifilisi nchi maskini. Ili kufahamu kwa kina chimbuko na maana ya tofauti hizo hatuna budi kuuelewa mfumo wa kiuchumi unaozalisha umaskini wa nchi moja na utajiri wa nchi nyingine. Mfumo huo ni mfumo wa ubepari. Ni kupitia mfumo wa ubepari ndipo Uingereza iliikalia Tanzania kama koloni lake, na hivyo kuidumaza Tanzania huku Uingereza ikiendelea kutajirika. Kwa maana hiyo, ili tuelewe vema mazingira yanayozalisha MIUMBI, hatuna budi kuuchambua kwanza mfumo wa ubepari, kwa sifa zake na historia yake.

**Ubepari**

Ubepari ni mfumo wa uzalishaji mali wa kinyonyaji uliojikita katika umiliki binafsi wa njia kuu za uzalishaji mali (viwanda, migodi, mabenki, n.k.). Shabaha kuu ya ubepari ni kupora rasilimali, kunyonya jasho la wavujajasho na kulimbikiza mali mikononi mwa mabepari wachache. Sifa za ubepari zimeainishwa hapa chini.

Mosi, ubepari ni mfumo wa uzalishaji mali wenye matabaka makuu mawili:

(i) *Tabaka la mabepari (wavunajasho)*: Hili ni tabaka linalomiliki njia kuu za uzalishaji mali (kama viwanda vikubwa, migodi mikubwa, mabenki makubwa, n.k). Mabepari huwa hawafanyi kazi bali wanafanyiwa kazi, kisha wao wanatwaa faida inayopatikana.

(ii) *Tabaka la wafanyakazi (wavujajasho)*: Hili ni tabaka lisilo na njia nyingine ya kuishi isipokuwa kwa kutumia nguvu-kazi

ya akili na mikono yake. Tabaka la wavujajasho halina nguvu ya mtaji ila lina nguvu kazi. Wanaofaidi matunda ya jasho la tabaka la wavujajasho ni mabepari, yaani wavunajasho.

Lipo tabaka jingine ambalo ni tabaka la kati, lenye wataalamu, ambao wengi wao huajiriwa katika taasisi mbalimbali zilizoanzishwa kwa ajili ya kuulinda na kuustawisha ubepari.

Pili, mfumo wa ubepari umetawaliwa na ulimbikizaji usio na kikomo wa ziada. Zipo njia kuu mbili za ulimbikizaji wa kibepari, ambazo ni:
(i) *Ulimbikizaji kwa njia ya uporaji*: unatumia mabavu ya dola, ikiwemo uvamizi wa kijeshi na njia nyingine za kiharamia, ili kupora nguvu kazi na rasilimali kutoka mikononi mwa wavujajasho na kuziweka mikononi mwa mabepari. Mahusiano kati ya nchi maskini na nchi tajiri yametawaliwa na mbinu hii.
(ii) *Ulimbikizaji kwa njia ya unyonyaji*: ambapo mabepari huchukua faida iliyozalishwa na wafanyakazi na kuirejesha tena katika uwekezaji ili kutanua nguvu yao. Mbinu hii hutumika zaidi ndani ya nchi tajiri.

Tatu, ubepari ni mfumo wa kidunia. Mfumo wa kidunia wa ubepari hujulikana kama ubeberu. Ubeberu ni ubepari uliokomaa na kuvuka mipaka ya nchi ulimozaliwa ili kunyonya jasho na kupora rasilimali za nchi zingine. Iwapo ubepari huzalisha matabaka baina ya watu ndani ya nchi, basi ubeberu huzalisha matabaka baina ya nchi katika mfumo wa kidunia. Nchi zinazounda mfumo wa kidunia wa kibepari

zimegawanyika katika makundi makuu mawili:

Kundi la kwanza ni la nchi tajiri, ambazo nyingi zake ni nchi za Magharibi kama Marekani, Uingereza, Kanada, Ujerumani, Ufaransa, Ubelgiji, Japan, n.k. Nchi hizi zina sifa kadhaa: (i) zina maendeleo makubwa ya kiteknolojia (ii) zinamiliki sehemu kubwa ya pato la dunia (iii) zina nguvu za kijeshi (iv) Kwa sehemu kubwa, watu wake wana maisha ya hali ya juu. Nchi hizi tajiri ndizo zimeutawala mfumo wa kidunia na ndizo zinazofaidika nao. Nchi hizi pia huitwa nchi za kibeberu au nchi za Kaskazini.

Kundi la pili ni la nchi maskini, ambazo pia hujulikana kama nchi za Kusini au nchi za pembezoni. Nyingi ya nchi hizi, zina utajiri asilia na rasilimali kama misitu, maziwa, madini, wanyamapori, ardhi yenye rutuba, n.k. lakini maendeleo yake ni duni. Kwa kweli, nchi hizi zinazidi kudumaa kimaendeleo. Sifa kuu za nchi za Kusini ni pamoja na:

(i) Hutegemea usafirishaji wa madini ghafi au mazao ghafi kwenda katika nchi zilizoendelea.
(ii) Hutegemea kuagiza bidhaa za viwandani kutoka katika nchi zilizoendelea. Hii ni kusema kwamba nchi hizi hazina ufungamano kati ya sekta ya kilimo na sekta ya viwanda. Kwa ufupi, ni nchi zinazozalisha zisichokitumia na zinatumia zisichokizalisha.
(iii) Hutegemea mitaji kutoka kwa mabepari wa ughaibuni
(iv) Zina maendeleo duni ya kiteknolojia
(v) Zina uchumi usioweza kujiendesha. Nchi hizi zina

matumizi makubwa kuliko mapato kwa sababu bidhaa za viwandani zinazoagizwa nje, zinazidi kupanda bei kila uchao ilhali bei ya malighafi huendelea kushuka. Hujikuta zikitegemea zaidi mikopo ambayo hutozwa riba kubwa, na misaada, ambayo huja kwa gharama ya uhuru wa nchi hizi kujiamulia mambo yake.
(vi) Hali ya maisha ya wananchi walio wengi ni duni sana, na wengi hufariki kwa maradhi yanayoweza kuzuilika.
(vii) Hazina tabaka la mabepari wa ndani wenye nguvu ya kiuchumi ya kushindana na mabepari wa kimataifa. Matokeo yake ni kuwa mabepari wa ndani hugeuka kuwa mawakala wa mabepari wa nchi za nje.

Lipo kundi la tatu linaloundwa na nchi chache ambazo zimepewa jina la nchi zinazoibukia (*emerging countries*). Hizi ni nchi kama China, India, Brazil na Afrika Kusini ambazo zinapiga hatua kutoka nchi maskini kuelekea nchi zilizoendelea. Hata hivyo, kwa sehemu kubwa, nchi hizi zimekuwa tu ni njia ambayo kampuni kubwa za Magharibi huitumia ili kuzinyonya na kuzipora nchi za Kusini.

Hii ni kusema kuwa nchi za kibeberu ndizo zinazonufaika zaidi na kutokuwepo kwa usawa katika mfumo wa kiuchumi wa kimataifa huku nchi za Kusini zikiwa ndizo nchi zinazopoteza zaidi ndani ya mfumo huo. Kwa hiyo, mkanganyiko wa msingi katika mfumo wa kidunia ni baina ya nchi za kibeberu kwa upande mmoja na nchi za Kusini kwa upande mwingine. Kwa kuwa bara la Afrika linaangukia katika nchi za Kusini basi ni vema kuielewa historia ya

mahusiano kati ya Afrika na nchi za kibeberu.

Mahusiano kati ya nchi za kibeberu na Afrika, yalianza karne ya 15, na yameshapitia vipindi vikuu vitatu:
(i) biashara ya utumwa na uporaji wa rasilimali, kati ya karne ya 15 na 19,
(ii) ukoloni mkongwe, kutoka katikati mwa karne ya 19 hadi katikati mwa karne ya 20.
(iii) ukoloni mamboleo kuanzia miaka ya 1960 hadi leo hii.

Ukoloni mamboleo pia umekuwa ukijibadili sura. Kwa muktadha uliokuwepo katika miaka ya mwanzo ya uhuru, nchi za Kiafrika zilipata fursa na ahueni ya kutekeleza sera za kizalendo na ustawi. Kuanzia miaka ya 1980 ukoloni mamboleo ulichukua sura ya uliberali mamboleo ambao uliiizuia Afrika kutekeleza sera za kizalendo na ustawi wa watu wake. Kipengele hiki kitafafanuliwa zaidi katika sura ya pili.

Licha ya kupitia vipindi tofauti tofauti, mahusiano kati ya Afrika na nchi za Ulaya kuanzia karne ya 15 hadi hivi sasa yametawaliwa na sifa za jumla ambazo zimejitokeza katika kipindi chote japo kwa viwango vinavyotofautiana. Sifa hizo ni pamoja na:
(i) uporaji wa rasilimali unaofanywa na kampuni kubwa za nchi za kibeberu
(ii) uvamizi wa kijeshi unaofanywa na majeshi ya nchi za kibeberu dhidi ya nchi maskini
(iii) amri, masharti, vitisho na vikwazo vinavyotolewa na

serikali za kibeberu, pamoja na taasisi zao kwa nchi maskini
(iv) kuwaondoa madarakani kwa hila viongozi wa nchi za Kusini waliodiriki kufuata na kutekeleza sera zinazokinzana na maslahi ya makampuni ya kibeberu na nchi zilizoendelea;
(v) biashara isiyo na usawa, ambayo inazifukarisha zaidi nchi maskini na kuzifaidisha nchi za kibeberu.
(vi) mfumo wa utengenezaji na usambazaji maarifa, kupitia vyombo vya habari, utamaduni na taasisi za kielimu, uliolenga kushusha hadhi ya utu wa watu wa nchi maskini na kuwafanya watukuze umagharibi/uzungu ili kushadadia ukandamizaji wa kihistoria unaofanywa na mataifa ya Ulaya dhidi ya nchi maskini
(vii) mikataba ya kilaghai na sheria za kimataifa zilizolenga kuzididimiza zaidi nchi maskini
(viii) uhodhi wa dola ya Marekani kama kipimo kikuu cha uimara na ubadilishaji wa fedha za nchi nyingine
(ix) mapambano ya watu wa nchi za Kusini dhidi ya unyonyaji na ukandamizaji unaofanywa na nchi za kibeberu.

Kwa kuwa mahusiano kati ya nchi tajiri na nchi maskini yanalindwa na sheria na mikataba ya kimataifa, ikiwemo mikataba ya MIUMBI, ni vema basi tukazitazama sheria za kimataifa na jinsi ambavyo zimekuwa zikitumika kulinda unyonyaji na ukandamizaji unaofanywa na nchi tajiri dhidi ya nchi maskini.

## Uibukaji wa Mikataba na Sheria za Kimataifa

Nyumba huwa na msingi pamoja na sehemu ya juu. Kama ilivyo nyumba, mfumo wa uzalishaji mali unaotawala katika jamii yoyote umeundwa na sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni msingi. Huu ni mfumo wa uchumi, ambao unahusisha nguvu na zana za uzalishaji-mali pamoja na mahusiano ya uzalishaji-mali. Sehemu ya pili ni mfumo wa kiitikadi ambao unaundwa na maarifa, sheria, maadili na amali za jamii husika. Msingi, ambao ni mfumo wa kiuchumi ndiyo huamua aina ya itikadi itakayotamalaki katika jamii. Kama mfumo wa uzalishaji-mali ni wa utumwa, basi mfumo wa maarifa, sheria, maadili hata mahubiri ya kidini katika jamii husika yatalenga kuhalalisha na kulinda utumwa. Kwa hiyo basi, kwa kuwa mfumo wa kimataifa wa kiuchumi ni wa kibepari, na umetawaliwa na ulimbikizaji wa kiporaji, basi sheria za kimataifa katika mfumo wa kibepari zimelenga kulinda na kuhalalisha unyonyaji, uporaji na ukandamizaji unaofanywa na mataifa yenye nguvu za kijeshi na kiuchumi dhidi ya mataifa maskini.

Wakati wa kipindi cha mpito kutoka katika mfumo wa ukabaila kwenda katika mfumo wa ubepari, huko Ulaya kulikuwa na muunganiko kati ya dola na kanisa, yaani dola na kanisa vilikuwa kitu kimoja. Kwa maana hiyo, kiongozi wa Kanisa Katoliki (Papa) ndiye aliyekuwa chanzo cha sheria za kimataifa kwani idhini yake ndiyo iliyohesabika kama sheria. Haishangazi kuwa tamko la Papa Nikolasi wa V lililotolewa tarehe 18 Juni 1452 (lililojulikana kama *Dum*

*Diversas*) lilimpatia Mfalme wa Ureno “idhini kamili na huru ya kuvamia, kutafuta, kukamata na kuwakalia Waislamu na wapagani na watu wowote wasioamini na maadui wa Kristo popote pale watakapokuwa, pamoja na majimbo, nchi, wilaya, na mali zingine zozote… na kuwageuza watu wa maeneo hayo kuwa watumwa wa milele.” Tangu mwaka 1441, Wareno walikuwa wameivamia Pwani ya Afrika Magharibi na kuwageuza Waafrika kuwa watumwa, hivyo tamko la Dum Diversas ambalo lilihesabika kama sheria ya kimataifa lilihalalisha udhalimu huo.

Tamko jingine la Papa lililojulikana kama *Romanus Pontifex* la mwaka 1455 liliimarisha zaidi tamko la awali (*Dum Diversas*), likiipatia Ureno haki na mamlaka ya kuyakalia maeneo ya Magharibi mwa Afrika, na kuwageuza Waafrika kuwa watumwa.

Papa Calixtus III, Sixtus IV na Leo X waliendelea kuthibitisha na kutumia matamko ya *Dum Diversas* na *Romanus Pontifex*. Hata Papa Alexander VI alitumia matamko hayo kama msingi wa kuruhusu Hispania kuvamia mabara ya Amerika, ambako mataifa ya Ulaya yaliwageuza wenyeji kuwa watumwa, na baadaye kuwaua kwa mamilioni huku wakipora ardhi yao na kuwaleta Waafrika kuwa watumwa katika mabara ya Amerika.

Kwa ufupi, sheria za kimataifa zilizowekwa kati ya karne ya 15 na 16 zilijenga misingi na kuhalalisha haki ya mataifa ya Ulaya kuvamia mabara mengine ya Afrika na Amerika, kuwauwa watu wa mabara hayo, kuwageuza watumwa, kuwapora

rasilimali zao na kutweza utu wao. Kwa kufanya hivyo, sheria hizo zilitumika kuimarisha mfumo mpya wa mahusiano ya kiuchumi kati ya Ulaya na mabara mengine, ambao ulifanya Ulaya kuwa kitovu cha mahusiano, wakati mabara mengine – ikiwemo Afrika – kuwa tegemezi kwa Ulaya.

Kwa mfano, wakati Wareno wanaivamia Pwani ya Afrika ya Magharibi katika karne ya 15, walikuta Waafrika wakitengeneza mahitaji ya kila aina – tangu nguo hata vyombo – na dola za Afrika Magharibi zikifanya biashara baina yao kwa kubadilishana bidhaa. Mbali na kuwawinda kwa mabavu Waafrika na kuwapeleka katika mabara ya Amerika kuwa watumwa, Wareno pia waliiteka mifumo ya kibiashara iliyokuwepo na wao wakawa ndio wafanyabiashara wakuu wakitoa bidhaa toka sehemu moja ya Afrika Magharibi kwenda nyingine. Kwa maana nyingine, katika hatua za awali Wareno walikuwa ni kama wasambazaji wa bidhaa zinazotengenezwa na Waafrika. Hata hivyo, baada ya kujiimarisha, Wareno na mataifa mengine ya Ulaya waliharibu mifumo hiyo na kuyageuza mahusiano ya Waafrika kuwa ni mahusiano kati ya Afrika na Ulaya, huku Ulaya ikiwa ndiyo kitovu cha uzalishaji wa bidhaa za viwanda na Afrika kuwa chanzo cha malighafi na masoko ya bidhaa zinazozalishwa Ulaya[1] . Hii ndio kusema kwamba uwezo wa kiteknolojia wa Waafrika kujizalishia mahitaji yao wenyewe na kufanya biashara baina yao ukawa umeharibiwa na uchumi wa Afrika ukageuzwa kuwa uchumi uchwara uliopo kwa ajili ya kutimiza

[1]Walter Rodney, *How Europe Underdeveloped Africa* (Washington, DC: Howard University Press, 1982), uk. 104

mahitaji ya Ulaya.

**Ukoloni na Mikataba ya Kilaghai**

Mataifa ya Ulaya yalipokuwa yakianzisha mahusiano na mabara mengine, yalikataa kuwatambua wenyeji wa mabara hayo kama binadamu kamili, bali nusu wanyama, wasio na chembe ya ustaarabu na wanaoishi katika ushirikina.

Hivyo, mahusiano kati ya wazungu na watu wa mabara hayo yalitawaliwa na yameendelea kutawaliwa kwa mabavu pamoja na ulaghai unaofanywa na Ulaya dhidi ya watu wa mataifa mengine. Baada ya miaka 400 ya kuliharibu Bara la Afrika kwa uvamizi na uporaji wa watu na rasilimali nyingine kupitia biashara ya utumwa, mataifa ya Ulaya yalifikia mapinduzi ya viwanda na hivyo kuamua kuanzisha ukoloni badala ya biashara ya utumwa. Kampuni za Ulaya zilizokuwa zikiongoza uvamizi wa bara la Afrika ili kuanzisha makoloni zilitumia mbinu mbalimbali ikiwemo kusaini mikataba ya kilaghai iliyosemekana kuridhiwa na watawala wa Kiafrika. Kwa kuwa kampuni hizo zilikuwa katika mashindano makali ya kuikalia Afrika, basi mikataba ya kilaghai ilikuwa ndiyo njia ya kuhalalisha madai ya taifa moja la Ulaya dhidi ya taifa jingine la Ulaya pale palipokuwa na ugomvi juu ya nani mmiliki halali wa eneo fulani la Afrika. Mfano wa mikataba hiyo ya kilaghai ni "mkataba wa Urafiki wa Kudumu" uliosemwa kusainiwa kati ya Karl Peters na Sultani Mangungo wa Msovero, tarehe 29 Novemba 1884.

Baadhi ya vipengele vya mkataba huo vinasomeka hivi:

> Mangungo, Sultani wa Msovero, Usagara, na Dkt. Karl Peters. Mangungo kwa niaba ya watu wake wote na Dkt. Peters kwa niaba ya wabia wake wa kibiashara wa sasa na wa baadaye wanaweka mkataba wa Urafiki wa Kudumu.
>
> Mangungo anaitoa nchi yake yote pamoja na mali za raia wake kwa Dkt. Karl Peters kama mwakilishi wa Kampuni ya Kijerumani ya Kujitafutia Makoloni kuwa koloni ya Ujerumani.
>
> Dkt. Karl Peters, kwa niaba ya Kampuni yake, amekubali kuitwaa nchi ya Sultani Mangungo na haki zake zote kuwa koloni la Ujerumani.

Chanzo: G.C.K. Gwasa, "The German Intervention and African Resistance in Tanzania" in A History of Tanzania, ed I.N. Kimambo and A.J. Temu (Nairobi: East African Publishing House, 1969), 99.

Ukitazama vipengele vya huo uitwao "mkataba wa urafiki wa kudumu" kati ya Karl Peters na Sultani Mangungo huwezi kukubali kuwa huu ni mkataba wa usawa. Kwanza, mkataba uliandikwa kwa Kijerumani, lugha ambayo Mangungo hakuifahamu. Pili, japokuwa inasemekana kulikuwa na mkalimani lakini mkalimani huyo aliajiriwa na Karl Peters, hivyo ni wazi kuwa alifuata matakwa ya Karl Peters, na ni vigumu kujiridhisha kuwa hakumpotosha Mangungo. Tatu, hata kama angevifahamu vipengele vya mkataba, Mangungo hakuwa na chaguo zaidi ya kukubali kuusaini la sivyo angeuawa na himaya yake kutwaliwa kwa nguvu. Karl Peters na maafisa wote waliokuja kuanzisha ukoloni walijulikana kwa ukatili wao dhidi ya Waafrika na walikuwa wakitumia majeshi kwa ajili ya kuvamia himaya za Waafrika zilizokataa kujisalimisha. Hayo yote ndiyo yanayoufanya mkataba huo kuwa wa kilaghai,

unaolenga kupora upande mmoja ili kuufaidisha upande mwingine. Hoja yetu kuu ni kwamba mikataba ya aina hiyo imeendelea kusainiwa hata baada ya Afrika kujipatia uhuru wa kisiasa kutoka kwa Wakoloni. Na Mikataba ya Uwekezaji kati ya Nchi Mbili (MIUMBI) ni mfano thabiti wa mikataba hiyo. Je, nchi za Kiafrika zitaendelea kuikumbatia mikataba hiyo au zitaikataa?

**Hitimisho**

Sura hii imefafanua maana na sifa za ubepari na ubeberu na kujadili mahusiano kati ya Afrika na nchi za kibeberu katika zama kuu mbili: zama za biashara ya utumwa na zama za ukoloni. Katika zama za biashara ya utumwa, sheria za kimataifa zilihalalisha nchi za Ulaya kuvamia mabara mengine, likiwemo bara la Afrika, na kupora watu wake pamoja na rasilimali zake. Uporaji huo ndio ulijenga msingi wa mahusiano kati ya nchi za Ulaya na Afrika ambapo Afrika ilifukarishwa na kugeuzwa kuwa tegemezi kwa nchi za Ulaya, kutokana na uchumi wake kuharibiwa. Utegemezi wa Afrika kwa nchi za Magharibi ulitawaliwa na ulimbikizaji wa kiporaji ambao uliitajirisha Ulaya na kuididimiza Afrika. Katika zama za ukoloni, kuliibuka mikataba ya kilaghai baina ya kampuni za kibeberu na watawala wa Afrika ambayo ilitumiwa na Ulaya kuhalalisha kuitawala Afrika na kupora rasilimali zake kupitia ukoloni. Ulimbikizaji wa kiporaji uliendelea na ulizidi kujenga utegemezi wa Afrika kwa Ulaya.

Zama hizo mbili zilikuwa muhimu kwa uibukaji na uimarikaji wa mfumo wa kidunia wa kibepari, ambao ndio chanzo cha nchi maskini na nchi tajiri. Ni katika zama hizo ndipo mifumo na misingi ya mahusiano ya kidunia ilitengenezewa sheria na desturi ambazo chimbuko lake ni Ulaya. Sheria na desturi nyingi zinazoendesha mahusiano baina ya nchi moja na nyingine au nchi za dunia kwa pamoja zilianzishwa wakati nchi nyingi za Kusini, zikiwemo nchi za Afrika, zikiwa hazijapata uhuru wake. Nchi za Kusini zilipopata uhuru zilikutana na sheria na desturi zinazoongoza mfumo wa kidunia ambazo misingi yake ni ubeberu. Na hata baadhi ya sheria zilizotungwa wakati nchi hizi zikiwa tayari ziko huru chimbuko na msukumo wake ni uleule wa kuendeleza na kukuza ubeberu duniani.

# SURA YA 2

# MAGEUZI YA SOKO HURIA NA UTITIRI WA MIUMBI

Sura ya kwanza ya kitabu hiki imefafanua tabia za mfumo wa ubepari na namna ambavyo mfumo huo ulitengeneza msingi wa kuibuka kwa sheria na mikataba ya kimataifa iliyohalalisha uporaji na unyonyaji uliofanywa na mataifa ya Ulaya kwa bara la Afrika. Sura hii ya pili imelenga kuchambua vipindi viwili vya ubepari wa kidunia. Cha kwanza ni kipindi cha ubepari wa kidunia uliopunguzwa makali ambacho mwanazuoni Samir Amin alikiita *negotiated globalization*[2] . Kipindi hiki kilianza mwaka 1945 na kuisha miaka ya 1970. Kisha kikafuatia kipindi cha utandawazi wa soko huria (*neoliberal globalisation*) kilichoanza miaka ya 1980 na kuendelea mpaka hivi sasa. Ni katika kipindi hiki cha pili, cha utandawazi wa soko huria, ndipo MIUMBI iliongezeka, ikitawala zaidi mahusiano kati ya nchi maskini na nchi tajiri.

## Zama za Ubepari Uliopunguzwa Makali

Kipindi cha ubepari uliopunguzwa makali kilianza mara

[2]Jipson John and Jitheesh P.M., "Globalisation and Its Alternative: An Interview with Samir Amin," *Tricontinental: Institute of Social Research* Political Notebook No. 1, Oktoba 29, 2018.

baada ya kumalizika kwa vita vikuu vya pili vya dunia mwaka 1945 hadi miaka ya 1970. Katika kipindi hiki, kulikuwa na mapambano kadhaa katika ngazi ya dunia, yaliyoulazimisha mfumo wa ubepari kufanya marekebisho na kutoa unafuu kwa nchi za pembezoni. Mapambano hayo yanajumuisha:

(a) Mapambano ya makoloni katika mabara ya Asia na Afrika kudai uhuru. Nchi za kibeberu zilijikuta hazina namna isipokuwa kutoa uhuru huo. Baada ya kupata uhuru, nchi maskini za Afrika, Asia na Amerika ya Kusini zilianza kudai mageuzi katika mfumo wa kiuchumi wa kimataifa. Nchi hizi ziliunda majukwaa mbalimbali, yakiwemo, *Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (Non Aligned Movement, NAM), Kundi la Nchi 77* (*G-77*), n.k. Majukwaa hayo yalitumika katika kupambana dhidi ya uonevu na unyonyaji uliokuwa ukifanywa na nchi tajiri dhidi ya nchi maskini. Ndani ya nchi za pembezoni zenyewe kulikuwa na sera za kitaifa zilizolenga kujenga uchumi unaojitegemea na kujenga usawa. Mfano wa sera hizo ni Azimio la Arusha lililopitishwa nchini Tanzania mwaka 1967 na kuipa serikali wajibu na mamlaka ya kutaifisha njia kuu za uzalishaji-mali na kuziweka katika mikono ya serikali. Nguzo kuu tano za kiitikadi za Azimio la Arusha ni:
(i) umiliki wa umma na udhibiti wa dola wa njia kuu za uzalishaji mali
(ii) kujitegemea kiuchumi
(iii) maendeleo vijijini
(iv) demokrasia ya umma, na
(v) miiko ya uongozi.

(b) Uwepo wa Urusi kama dola la kijamaa lenye nguvu za kijeshi na kiuchumi, ambalo kambi yake pia ilijumuisha nchi za Ulaya Mashariki. Urusi ilitoa mbadala kwa nchi zilizopinga ubeberu ili zisiteketezwe na mabeberu.
(c) Mapinduzi ya kijamaa katika baadhi ya nchi kama vile China, Korea Kaskazini, Cuba na Vietnam ambayo yalikuwa tishio kubwa kwa mfumo wa ubepari duniani.
(d) Harakati za vyama vya wafanyakazi katika nchi za kibeberu, zilizojumuisha pia vuguvugu la watu weusi kupinga ubaguzi wa rangi pamoja na mavuguvugu ya kupinga uvamizi wa kijeshi uliokuwa ukifanywa na nchi za kibeberu dhidi ya nchi za Kusini.

Kutokana na harakati hizo za kimapinduzi, mabepari wa kimataifa pamoja na serikali zao hawakuwa na namna zaidi ya kufanya mageuzi katika mfumo wa ubepari. Ndani ya nchi za kibeberu zenyewe zikaanzishwa sera za ustawi (*welfare policies*) zilizotoa unafuu kwa tabaka la wafanyakazi ili kuzuia tabaka hilo lisilete mapinduzi ya kijamaa. Pili, katika ngazi ya kidunia, ubeberu ulilazimishwa *kuvumilia* sera za kitaifa zilizoanzishwa na nchi maskini. Baadhi ya nguzo za sera hizo za kitaifa zilikuwa:
(i) utaifishaji wa njia kuu za uchumi
(ii) utoaji wa huduma za kijamii kwa wote bila malipo
(iii) uanzishaji wa viwanda vya kupunguza utegemezi wa bidhaa za nje yaani *import substitution industrialisation.*
(iv) dola kuingilia katika uchumi ili kuzuia mporomoko wa bei, kulinda soko la ndani, kuratibu shughuli za kampuni za kimataifa, n.k

(v) kuwa na nguvu ya maamuzi katika vyombo vya kimataifa, pamoja na nguvu ya kupanga bei za bidhaa zinazozalishwa katika nchi maskini.
(vi) Mfumo na vyombo vya kisheria vya ndani ya nchi maskini ndivyo vitumike katika utatuzi wa migogoro baina ya kampuni za ughaibuni na nchi maskini.

Sera za kitaifa zilizotajwa hapo juu kwa ujumla wake zina mwelekeo wa ujenzi wa uchumi wa kitaifa. Uchumi wa kitaifa ni uchumi ambao umejinasua kutoka katika utegemezi wa nje kwa kufungamanisha sekta zake za ndani za uzalishaji na sekta zake za ndani za utumiaji. Siyo kwamba nchi maskini zilifanikiwa kujenga uchumi wa kitaifa, la hasha! Lakini walau nafasi ilikuwepo ya kujaribu kupunguza utegemezi wa nje. Zaidi ya hapo, ubeberu ukalazimishwa kukubaliana na matakwa matatu ya nchi za pembezoni ambayo ni haki ya nchi kujiamulia mambo yake yenyewe, utaifishaji wa njia kuu za uchumi, na majaribio ya kujenga uchumi unaojitegemea.

Nchi za Kusini pia zilipigania nafasi ya kubadili mfumo wa uendeshaji uchumi na siasa za dunia ikiwemo namna maamuzi yanavyofanyika katika taasisi za kimataifa. Hii ilikuwa ni njia ya kusukuma kupatikana kwa usawa na haki zaidi katika uchumi na siasa za kimataifa. Japokuwa hazikufanikiwa kubadili mfumo wa maamuzi katika taasisi za kiuchumi kama Benki ya Dunia na Shirika la Kimataifa la Fedha, nchi maskini ziliweza kushawishi kupitishwa kwa maazimio katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa yaliyotambua madai yao. Mojawapo ya maazimio hayo ni Azimio 1803 (XVII)

la mwaka 1962 lililosimika mamlaka ya kudumu ya nchi maskini juu ya rasilimali na utajiri asilia unaopatikana katika nchi hizo. Hata hivyo azimio hilo lilitaja sheria za kimataifa kutumika sambamba na sheria za nchi maskini kuamua kuhusu fidia inayopaswa kulipwa kwa kampuni ambayo mali zake zimetaifishwa.

Mwaka 1974, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha maazimio mengine mawili ambayo ni Mkataba wa Haki na Wajibu wa Kiuchumi wa Dola wa mwaka 1974 (*Charter of Economic Rights and Duties of States – CERDS*) na Tamko kuhusu Uanzishwaji wa Mfumo Mpya wa Kimataifa wa Kiuchumi (*Declaration on the New International Economic Order – NIEO*). Maazimio haya mawili yalienda mbali zaidi katika kutambua mamlaka ya kudumu ya nchi za Kusini juu ya utajiri asilia na rasilimali zao kwani yaliweka bayana kuwa ni sheria za ndani za nchi za Kusini ndizo zitakazotumika kuamua kiasi cha fidia na kutatua migogoro yoyote itakayoibuka kutokana na nchi maskini kutaifisha mali zilizokuwa zikimilikiwa na kampuni ya kigeni.

Hata hivyo, nchi za Magharibi zilikataa kutambua maazimio ya CERDS na NIEO kama sheria za kimataifa, zikidai kwamba nchi tajiri hazikuyaunga mkono maazimio hayo. Majaji katika mahakama za kimataifa kama ICJ nao walikataa kuyatambua maazimio hayo kama sehemu ya sheria za kimapokeo za kimataifa, na hivyo kushiriki kudidimiza mamlaka ya kudumu ya nchi maskini juu ya utajiri asilia na rasilimali zake. Kwa kuwa nguvu yao katika vyombo vya

kimataifa ilikuwa imepunguzwa kwa kiasi fulani, nchi tajiri zilianza kusaini mikataba ya uwekezaji kati ya nchi mbili (MIUMBI) na maskini. "Nchi hizo zinazosafirisha mtaji zilifanya jitihada za pamoja kusaini mikataba ya ubia kati ya nchi mbili [kati ya nchi tajiri na nchi maskini] ambayo ilikuwa na vifungu vilivyopingana kabisa na hatua za NIEO."[3] Kama itakavyofafanuliwa katika vipengele vinavyofuatia, idadi ya MIUMBI katika miaka ya 1960 na 1970 ilikuwa ndogo sana lakini iliongezeka katika miaka ya 1980 na kupaa zaidi kuanzia miaka ya 1990. Kasi hii ilitokana na mabadiliko ya kiuchumi yaliyotokea duniani yaliyozipatia nguvu zaidi kampuni za kimataifa pamoja na nchi za kibeberu.

**Ubepari wa Soko Huria**

Kuanzia miaka ya 1970, kulianza kutokea zahma katika mfumo wa kidunia wa ubepari. Ulimbikizaji uliokithiri katika nchi za kibeberu ulianza kusababisha mdororo wa kiuchumi, hali iliyofanya uchumi wa nchi tajiri kuanza kuporomoka. Kuanzia miaka ya 1980, mabepari waliitumia fursa hiyo ya zahma katika mfumo wa kibepari kusukuma mageuzi ambayo yalirudisha nguvu, mamlaka na faida mikononi mwa mabepari na nchi za kibeberu. Mageuzi hayo yalijulikana kama *uliberali mamboleo* au *soko huria*. Ndani ya nchi za Magharibi, mabepari waliondoa sera za ustawi, hali iliyosababisha ufukara mkubwa kwa tabaka la wafanyakazi. Katika mfumo wa kimataifa, mabepari wa nchi za Magharibi, wakishirikiana na serikali za

[3]Kate Miles, *The Origin of International Investment Law: Empire, Environment and the Safeguarding of Capital* (Cambridge: Cambridge University Press, 2013), uk. 100.

nchi zao pamoja na mashirika ya kimataifa, walizishinikiza nchi maskini kufanya mageuzi ya soko huria. Kwa kufanya hivyo, walishambulia sera za kitaifa zilizokuwa zikitekelezwa katika nchi maskini na kufanikiwa kuzizika. Baadhi ya nguzo[4] za mageuzi ya soko huria ni:

(a) *Ubinafsishaji:* Mashirika yote yanayomilikiwa na dola vikiwemo viwanda, huwekwa mikononi mwa watu binafsi. Hatua hii hulipotezea dola faida iliyopatikana katika shughuli za kiuchumi. Pia, kwa uzoefu wa Tanzania, sera za ubinafsishaji zilipelekea watu wengi sana kupoteza ajira kwani viwanda vingi vilivyobinafsishwa vilifungwa na kugeuzwa maghala ya kuhifadhia bidhaa kutoka nje. Hali hii pia iliongeza utegemezi kwa nchi za nje kwani bidhaa ambazo zilizalishwa ndani ilibidi ziagizwe kutoka nje.

(b) *Ulegezaji (liberalisation):* Dola hutakiwa kujiondoa katika uchumi. Kwa maana hiyo, dola huzuiliwa kulinda soko la ndani, kudhibiti bei na kulinda haki za wafanyakazi. Hatua hii huua viwanda vya ndani, hupelekea soko la ndani kujazwa na bidhaa toka nje, na hudhoofisha nguvu ya vyama vya wafanyakazi. Matokeo yake ni kuwa kampuni za kibepari hupata nguvu zaidi ya kuchota rasilimali, kupanga bei na kuwanyonya wafanyakazi.

(c) *Ubidhaishaji (commodification)*: Dola hulazimishwa kujiondoa katika utoaji wa ruzuku na huduma za kijamii kwa watu wake.

[4]Issa G. Shivji, *Accumulation in an African Periphery: A Theoretical Framework* (Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers, 2009)..

Huo ndio ukawa mwanzo wa huduma za msingi kugeuzwa kuwa bidhaa zinazouzwa sokoni na yeyote aliyezihitaji alitakiwa kuzinunua sokoni. Kadhalika, ruzuku za aina mbalimbali zikiwemo za mbolea kwa wakulima hata zile za chakula kwa wakazi wa mijini zilitakiwa kuondolewa. Hali hii ilididimiza maisha ya wananchi wa tabaka la chini pamoja na kudumaza uzalishaji katika kilimo.

(d) *Ufedhaishaji (financialisation)*: Dola hutakiwa kujiondoa katika kuratibu mfumo wa fedha pamoja na taasisi za kifedha. Hali iliyohalalisha ulanguzi wa fedha pamoja na kuruhusu utoroshaji wa mitaji na ziada iliyozalishwa katika nchi maskini kwenda katika nchi zilizoendelea.

(e) *Uwekezaji toka ughaibuni (FDI)*: Dola hutakiwa kuvutia wawekezaji kutoka ughaibuni kwa kutunga sera na sheria zenye kutoa vivutio kwa wawekezaji, kama misamaha ya kodi na ruhusa ya kuhamisha ziada iliyozalishwa nchini.

(f) *Mikopo na misaada yenye masharti:* Mikopo na misaada kutoka ughaibuni ilibeba masharti magumu kwa nchi maskini ambayo yalizitaka kufanya mabadiliko ya sera na sheria ili kuzatiti ubepari wa soko huria. Sera na sheria nyingi zilitungwa na wataalamu toka nchi za Magharibi waliotumwa na nchi zao au mashirika ya kimataifa kwa ajili ya kuleta mageuzi katika nchi maskini.

Hatua hizi za mageuzi ya soko huria, kwa ujumla wake, zinaimarisha zaidi ulimbikizaji wa kiporaji wenye mwelekeo

wa utegemezi kutoka nje. Kwa maana nyingine, uchumi unaojengwa siyo tena uchumi wa kitaifa bali ni uchumi wa kiwakala ambapo nchi za Kusini zinazidi kurejeshwa kuwa mashamba ya kuzalisha malighafi na masoko ya kuuza bidhaa zilizozalishwa nje. Kwa maana nyingine, watu wa nchi maskini hurudishwa katika hali ile ile iliyokuwepo wakati wa ukoloni ya kukata miwa na kuchuma pamba ili kusafirisha nje, kisha kuletewa nguo zilizokwishavaliwa (mitumba) pamoja na sukari ya daraja la chini kutoka nje. Katika uwanda wa siasa, nchi maskini zilipoteza haki ya nchi kujiamulia mambo yake yenyewe, na hasa uhuru wa kutunga sera na sheria zinazoendana na mahitaji ya watu wao pamoja na kulinda rasilimali zao kwa manufaa yao wenyewe. Kitabaka, sera hizi ziliwafukarisha zaidi wavujajasho na kuwapotezea haki ya kupata huduma za msingi bila malipo pamoja na kuua nguvu yao ya kimapambano. Matabaka ya mabepari wa nje, pamoja na vibaraka wao katika nchi maskini, ndio wamekuwa wafaidika wakuu wa sera hizi.

**Utitiri wa MIUMBI**

Mkataba wa kwanza wa MIUMBI ulisainiwa kati ya Ujerumani na Pakistani mwaka 1959. Mwaka huo huo, Ujerumani ilisaini mkataba mwingine na Jamhuri ya Dominika. Katika muongo mzima wa miaka ya 1960, MIUMBI iliyosainiwa ilikuwa 75 tu. Kati ya MIUMBI hiyo 75, MIUMBI 72 ilihusisha nchi za Magharibi na nchi maskini. Katika muongo wa miaka ya 1970, mikataba ya MIUMBI iliongezeka taratibu na kufikia 167, huku MIUMBI 153 kati ya hiyo ikihusisha nchi za Magharibi na nchi maskini. Idadi ya MIUMBI iliendelea

kuongezeka taratibu na kufikia 386 miaka ya 1980 huku asilimia 83 ya MIUMBI hiyo ikihusisha nchi za Magharibi na nchi maskini. Kati ya mwaka 1990 na 1996 pekee, idadi ya MIUMBI iliyosainiwa ilipaa na kufikia 1330 huku MIUMBI 822 kati ya hiyo ikihusisha nchi za Magharibi na nchi maskini[5] . Kasi ikaongezeka zaidi kuanzia miaka ya 1990 na kupaisha idadi ya MIUMBI kufikia 2608 mwaka 2008. Idadi hiyo iliendelea kuongezeka na kufikia 3,324 mwaka 2016.

Kama ilivyodokezwa hapo awali, kupaa huku kwa idadi ya MIUMBI kulitokana na mageuzi ya kiuchumi ya soko huria ambayo yalizipatia nguvu zaidi kampuni za kimataifa pamoja na nchi za Magharibi dhidi ya nchi maskini na watu wake. Hivyo, MIUMBI ikawa ni mojawapo ya nyenzo za kisheria zilizolinda mfumo mpya wa soko huria. MIUMBI ina vipengele vinavyozuia nchi maskini kuchukua hatua zozote zinazolenga kuratibu na kudhibiti shughuli za kampuni za uwekezaji na inazipatia kampuni hizo haki na mamlaka ya kushtaki nchi maskini katika vyombo vya kimataifa. Vipengele hivi pamoja na athari zake vitajadiliwa kwa kina katika sura inayofuata.

[5]UNCTAD, *World Investment Report 1997: Transnational Corporations, Market Structure and Competition Policy* (New York & Geneva: UNCTAD, 1997), uk. 19.

# SURA YA 3

# VIPENGELE MAHUSUSI VYA MIUMBI

Sura iliyotangulia imeonyesha kuwa katika miongo miwili ya mwanzo baada ya nchi za Afrika kujipatia uhuru (miaka ya 1960 na 1970), nchi za Kiafrika, zikishirikiana na nchi za Asia na Amerika ya Kusini, zilipambana kupunguza makali ya ubeberu kwa kutekeleza sera za kitaifa zilizolenga kuongeza uwezo wa nchi hizo kujiamulia mambo yake zenyewe, kujenga uchumi unaojitegemea pamoja na kulinda na kutumia rasilimali zao kwa faida yao wenyewe. Mapambano hayo yalipunguza unyonyaji wa nguvu-kazi na uporaji wa rasilimali uliokuwa ukifanywa nchi za Magharibi. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1980, nchi za Magharibi zilianza kupambana kurejesha nguvu yao ya awali na njia mojawapo ya kufanya hivyo ilikuwa kuingia mikataba na nchi za Kusini kwa lengo la kulinda mitaji yake na kuhakikisha kuwa faida inarudi katika nchi za Magharibi. Kama ambavyo imeonyeshwa mwishoni mwa sura ya pili, MIUMBI iliongezeka kwa kasi baada ya kuanza kwa mageuzi ya soko huria miaka ya 1980.

Sura hii ya tatu imelenga kufafanua vipengele vikuu vya MIUMBI na kuonyesha athari zake kwa taratibu za kisheria na uhuru wa nchi za Kusini kujiamulia mambo yao zenyewe, ikiwemo kulinda rasilimali zao na kuchagua sera za maendeleo zenye manufaa kwao.

**Vipengele Vikuu vya MIUMBI**

MIUMBI ina nguzo kuu nne: uhamasishaji wa uwezekaji wa moja kwa moja (foreign direct investment – FDI), upendeleo kwa wawekezaji, uhamishaji faida na utatuzi wa migogoro kimataifa. Japokuwa watetezi wa MIUMBI hudai kuwa mikataba hiyo husaidia kukuza uwekezaji na biashara, uchambuzi wa vipengele vyake unaonyesha kuwa vina athari kubwa kwa uchumi, utawala wa sheria na demokrasia kwa upande wa nchi za Kusini. Licha ya MIUMBI kuingiwa na nchi mbili, ni wawekezaji binafsi toka kwenye nchi zenye nguvu ya kiuchumi ndio huitumia kwa minajili ya kulinda mitaji yao katika nchi za Kusini. Kwa kuwapatia nguvu wawekezaji dhidi ya dola, MIUMBI hudhoofisha uhuru na mamlaka ya kuboresha sera na sheria pamoja na kukwamisha mifumo ya utoaji haki. Takribani MIUMBI inaweka wajibu kwa kila nchi kulinda na kuendeleza wawekezaji binafsi bila kutoa wajibu mahususi kwa wawekezaji kwa nchi walimowekeza.

Baadhi ya vipengele vinavyotoa upendeleo kwa wawekezaji vimefafanuliwa hapa chini.

### (i) Kuzuia Utwaaji wa Mali au Huduma bila Fidia (*Expropriation*)

MIUMBI inazuia nchi kutwaa mali za wawekezaji au kufanya maamuzi yanayoathiri wawekezaji au hata kupunguza mapato yanayotokana na uwekezaji wao. Katika medani ya sheria za kimataifa, kuna utwaaji wa aina mbili: utwaaji wa moja kwa moja na utwaaji usio wa moja kwa moja.

Utwaaji wa mali wa moja kwa moja (*direct expropriation*) hutokea pale dola linapochukua umiliki wa sekta ya kiuchumi au vifaa na mali inayotumika kuzalisha faida. Baadhi ya MIUMBI na sheria za kimatifa inatoa nafasi, japokuwa ni finyu, ya utaifishaji kufanyika kwa sharti kwamba utaifishaji huo uwe ni kwa ajili ya maslahi ya taifa (*national interest*), usiwe wa kibaguzi na uambatane na kutolewa kwa fidia ya papo kwa hapo kwa kuzingatia haki na usawa (*fair and equitable compensation*). Tafsiri hii inaleta changamoto juu ya kupata uwiano kati ya maslahi ya taifa na maslahi binafsi ya kibiashara. Mara nyingi kampuni hudai fidia kubwa, ikiwemo thamani ya mtaji kwa bei ya soko pamoja na faida ya baadaye. Aina hii ya madai ya fidia inapingwa na wachambuzi wanaounga mkono utaifishaji wakisema kuwa malipo ya fidia kwa mwekezaji yanapaswa kuwa sawa na kiwango halisi cha fedha ambacho wamiliki wa kampuni husika wamewekeza na siyo zaidi ya hapo[6].

[6]David Hall, "We've Crunched the Numbers–Nationalisation Would be a Bargain," *The Guardian*, Desemba 9, 2019. Imepatikana Oktoba 20, 2020 kutoka https://www.theguardian.com/commentisfree/2019/dec/09/numbers-public-ownership-uk-utilities-nationalisation

Aina ya pili ya utwaaji unaopigwa marufuku katika MIUMBI ni ule usio wa moja kwa moja (*indirect expropriation*). Huu huhesabika kutokea pale dola linapoamua kuchukua hatua za kudhibiti shughuli za kiuchumi. Mfano mzuri ni pale dola linapopitisha sheria na kanuni zinaongeza wajibu, ikiwemo ongezeko la gharama, kwa wawekezaji au kuondoa haki kwa mwekezaji kinyume na makubaliano ya awali. Kwa maana hiyo, iwapo nchi ya Kusini itaamua kupitisha sheria kubadili mfumo wa kodi, ambao itaondoa msamaha wa kodi kwa wawekezaji ili kuongeza mapato ya serikali, basi mwekezaji huyo anaweza kuishtaki nchi husika akidai fidia kwa sababu sheria hiyo mpya ya kodi huhesabika kama utwaaji usio wa moja kwa moja.

Pia, tafsiri ya utwaaji usio wa moja kwa moja hujumuisha hatua nyingine zozote zilizochukuliwa na dola ambazo huonekana kuwa na athari sawa na utwaaji usio wa moja kwa moja. Hii ni kusema kuwa hata kama hatua zilizochukuliwa na dola hazikulenga kabisa uwekezaji fulani, bado wamiliki wa uwekezaji husika wanaweza kulishitaki dola na kudai fidia kutokana na hasara waliyoipata[7].

Kwa kifupi, kipengele hiki cha MIUMBI kinazuia siyo tu utaifishaji bali hata udhibiti wa dola katika uchumi. Kwa upande mmoja, zuio hilo linatoa haki kwa wamiliki wa mtaji kuchuma faida bila kudhibitiwa na, kwa upande wa pili,

[7]Suzy H. Nikièma, *Best Practices: Indirect Expropriation* (Manitoba: International Institute for Sustainable Development, 2012), uk. 5

linapunguza nguvu ya dola kufanya maamuzi ya kisera na kuchukua hatua za kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

**(ii) Kuhakikisha Haki na Usawa (*Fair and Equitable Treatment – FET*)**

Kipengele cha Kuhakikisha Haki na Usawa kinalenga kutoa ulinzi kamili kwa mwekezaji anapokuwa ndani ya nchi. Nchi inayopokea uwekezaji inapaswa kuondoa ubaguzi na uonevu kwa kuweka vipimo vya kuthibitisha nia njema (*good faith*) na kwa mizania ya wanavyotendewa wawekezaji wengine (*proportionality*). Kwa maana nyingine, mwekezaji kutoka nchi iliyosaini MIUMBI anapaswa kupewa upendeleo usiopungua ule anaopewa mwekezaji wa ndani. Hatua yoyote itakayoonekana kumbagua mwekezaji au kwenda kinyume na makubaliano ya awali katika kumiliki na kufaidi matunda ya uwekezaji inaweza kupelekea mgogoro wa kisheria chini ya MIUMBI. Nchi nyingi zimekabiliwa na tuhuma za upendeleo na kufikishwa katika mahakama za kimataifa kwa sababu ya ukiukwaji wa kipengele hiki.

Kipengele hiki hutoa haki kwa mwekezaji na wajibu kwa nchi inayopokea mtaji. Nchi inayopokea mtaji haijapewa haki ya kumchukulia hatua mwekezaji anayekiuka masharti ya uwekezaji, haki za binadamu, uchafuzi wa mazingira au kuhatarisha usalama wa nchi hiyo. Ni dhahiri kuwa lengo kuu ni kulinda uwekezaji wa moja kwa moja (*foreign direct investment*) na maslahi ya nchi zinazosafirisha mtaji bila kulinda haki na maslahi ya nchi zinazopokea mtaji. Kadhalika, kipengele hiki

kinazuia nchi ya Kusini kuchukua hatua za upendeleo kwa wawekezaji wa ndani kwani kitendo hicho hutafsiriwa kama ubaguzi kwa wawekezaji toka nchi iliyosaini MIUMBI. Kwa maana hiyo, kupitia kipengele hiki, nchi ya Kusini inaweza kushtakiwa kwa kutoa nafasi za upendeleo kwa wawekezaji wa ndani au pale serikali inapojiingiza katika biashara ili kunufaika na rasilimali zake.

(iii) **Upendeleo Kutokana na Utaifa (*Most-Favored-Nation Treatment – MFN*)**

Kipengele hiki, ambacho kina historia ndefu kwenye mikataba ya biashara na uwekezaji, kinalenga kuzuia upendeleo mahususi ili kuongeza usawa na uwiano kati ya wawekezaji toka ughaibuni katika nchi inayopokea mtaji. Kwa mujibu wa kipengele hiki, wawekezaji kutoka nchi iliyosaini MIUMBI watafaidika moja kwa moja na upendeleo wowote unaotolewa kwa wawekezaji kutoka nchi nyingine.

Kipengele hiki kina utata mkubwa kwenye tafsiri yake wakati wa migogoro. Idadi kubwa ya MIUMBI haisemi kama dhana hii ya upendeleo inajumuisha sharti la kutolewa kwa fursa ya usawa na haki au ulinzi dhidi ya kutaifishwa kwa mali. Pia, MIUMBI iliyo mingi haiweki wazi kama makubaliano ya kibiashara katika jumuiya za kiuchumi kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) nayo yanahesabiwa kama upendeleo usio wa haki chini ya kipengele hiki.

Nchi inayozingatia kipengele hiki inakuwa imefungua mlango kwa uwekezaji holela kwa sababu haitaki kushitakiwa kubagua

wawekezaji kwa kutumia utaifa. Ni wazi kuwa kwa kupitia kipengele hiki, nchi maskini kama Tanzania itashindwa kulinda na kuendeleza viwanda vya ndani au kukuza uchumi wa kilimo kwa kuweka vivutio mahususi kwa wawekezaji wa ndani au nchi rafiki ya Kusini.

Kwa kifupi, kipengele hiki kinazinyima nchi za Kusini zilizosaini MIUMBI uhuru wa kufanya maamuzi ya kisheria na kisera yaliyo na manufaa kwa nchi, kanda au bara zima kwa kuhofia kushtakiwa na wawekezaji.

**(iv) Utatuzi wa Migogoro (*Dispute Resolution*)**

Katika suala la utatuzi wa migogoro, MIUMBI ina tofauti kubwa na mikataba mingine ya kimataifa kwa sababu MIUMBI inawapatia watu binafsi au kampuni binafsi haki ya kuishitaki nchi. Haki hiyo hutolewa kwa watu au kampuni binafsi licha ya kuwa wao siyo sehemu ya waliosaini au kuridhia MIUMBI husika.

Sehemu kubwa ya MIUMBI inazuia kutumia mahakama za ndani ya nchi inayopokea uwekezaji kwa kisingizio kuwa mahakama hizo hazina uhuru wala weledi wa kutoa maamuzi ya haki. Hii inatokana na madai kwamba nchi nyingi za Kusini zina muingiliano kati ya serikali na mfumo wa mahakama. Kwa mantiki hiyo, MIUMBI iliyo mingi hutaka mifumo ya kimataifa ndio itumike kutatua migogoro kati ya wawekezaji na serikali. Pande zote mbili zinawajibika kuainisha ni aina gani ya mifumo ya kimataifa itakayotumika itakapotokea mgogoro kati yao.

Nchi nyingi zinafuata mwongozo uliowekwa chini ya Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji kijulikanacho kwa Kiingereza kama *International Centre for Settlement of Investment Disputes* (*ICSID*). Kituo hiki kinatoa kanuni na taratibu za kusikiliza migogoro pamoja na huduma ya uendeshaji wa taratibu hizi. Mahakama ya ICSID ina mamlaka kisheria ya kutoa adhabu ikiwemo fidia au maelekezo kwa ajili ya kumaliza mgogoro.

Mfumo wa ICSID unavutia zaidi wawekezaji ambao hudai kuwa unawapa uhakika wa ulinzi wa mali zao dhidi ya serikali. Ni vema kutambua kuwa mfumo huu wa utatuzi wa migogoro ulianza miaka ya 1960 ili kulinda mali na biashara za nchi za kigeni zilizochumwa wakati wa ukoloni. Wakati nchi za Afrika zikijinyakulia uhuru, kulikuwa na hofu kuwa nchi nyingi zingetaifisha mali hizo zilizopatikana kwa njia ya uporaji wakati wa ukoloni. Hivyo, wamiliki wa kampuni za kigeni walijenga hoja kuwa wasingeweza kupata haki kwa kutumia mifumo ya ndani ya nchi kwa kuwa nchi changa za Afrika na Asia hazikuwa na uwezo wa kimahakama wa utoaji haki. Kwa hiyo, waliomba kutumia mifumo ya kimataifa iliyoko nje ya nchi hizo.

Licha ya kupita miongo zaidi ya sita baada ya nchi za Afrika kujipatia uhuru, madai ya wawekezaji wa kigeni ya kutokuwepo kwa uhuru ndani ya mifumo ya utoaji haki bado yameendelea kuwepo. Ni wazi kuwa wawekezaji wa kigeni wanatumia madai haya kama njia ya kuuwekea ulinzi mfumo wa ubepari wa kidunia unaowawezesha kuchuma mali katika

nchi maskini. Uzoefu umeonyesha kuwa uendeshaji wa mashauri katika mahakama za kimataifa unatoa upendeleo mkubwa kwa kampuni za kigeni bila kujali athari za kiuchumi na kijamii kwa nchi maskini. Kwa hiyo, lengo la mahakama hizi siyo kutoa haki kwa usawa bali kulinda utajiri wa kampuni za kigeni na nchi zinamotokea, utajiri uliopatikana kwa kutumia nguvu na ulaghai wakati wa ukoloni na kulindwa kwa kutumia mifumo ya sheria za kimataifa baada ya uhuru.

**(v) Uhamishaji wa Mitaji na Faida**

MIUMBI mingi imeweka vipengele vinavyowapatia wawekezaji haki ya kuhamisha mitaji na faida waliyochuma katika nchi zinazopokea mtaji bila vikwazo au kucheleweshwa. Uhamishaji huo hufanyika kwa fedha za kigeni na hata wakati mwingine kwa kiwango fulani cha kubadilishia fedha ili kulinda mitaji dhidi ya mfumuko wa bei[8]. Taratibu za kuingiza na kuhamisha mitaji hutumika kama kipimo cha mazingira bora ya biashara na uwekezaji katika nchi. Baadhi ya MIUMBI huwalinda wawekezaji dhidi ya sheria za usimamizi wa fedha zikiwemo za ufilisi au zile zinazolenga kudhibiti uhamishaji holela wa fedha kwenda nje ili kuhakikisha kuwa fedha zinabakia katika benki za ndani kwa ajili ya kuimarisha uchumi.

Fedha nyingi kuingia au kutoka ndani ya nchi bila utaratibu maalum huwa na athari kubwa sana kwa uchumi mpana.

[8]Rudolf Adlung na Martin Molinuevo, "Bilateralism in Services Trade: Is There Fire behind the (BIT-) Smoke?" *Journal of International Economic Law* 11, No. 2 (June 2008).

Kwa maana hiyo, usimamizi wa fedha za kigeni na udhibiti wa utoroshaji wa mitaji ni nguzo muhimu katika kuimarisha uchumi. Kipengele cha MIUMBI kinachozuia nchi zinazopokea mitaji kudhibiti uhamishaji wa fedha na mitaji kina nia ya kuendeleza unyonyaji unaofanywa na nchi za Magharibi kwa nchi za Kusini kwa kudhoofisha uwezo wa nchi hizo kujenga uchumi imara. Athari kuu kwa nchi maskini kutokuwa na kwa utaratibu mzuri wa kudhibiti uhamishaji wa fedha na mitaji ni kuongezeka kwa umaskini, utegemezi na madeni licha ya nchi husika kuruhusu uvunaji holela wa rasilimali zake.

Utafiti uliochapishwa na Chuo Kikuu cha Massachusetts mwaka 2021 unaonyesha kuwa nchi 30 za Afrika (ikiwemo Tanzania) zilipoteza kwa pamoja takribani dola za Marekani trilioni 2 (sawa na Sh trilioni 4,656) kati ya mwaka 1970 na 2018 kupitia utoroshaji wa fedha, ambao huwezekana kwa sababu nchi za Afrika zimezuiliwa kudhibiti uhamishaji wa fedha[9]. Sehemu kubwa ya utoroshaji huo hufanywa na kampuni za uwekezaji kutoka ughaibuni kupitia udanganyifu wa bei na thamani halisi ya bidhaa (*trade misinvoicing*) na umekithiri zaidi katika sekta za uchimbaji wa madini na mafuta. Kiasi kilichotoroshwa kutoka Afrika ni kikubwa zaidi ya fedha zilizokopwa na nchi hizo za Afrika katika kipindi husika, ambazo ni dola za Marekani bilioni 720 (takribani Sh

[9]Léonce Ndikumana na Joyce K. Boyce, "Capital Flight From Africa 1970–2018: New Estimates with Updated Trade Misinvoicing Methodology," PERI Research Report (Amhrest: University of Massachusetts Amhrest, 2021).

trilioni 1,676). Tanzania pekee ilipoteza dola za Marekani bilioni 42 (takribani Sh trilioni 97.8) zilizotoroshwa kwenda nje ya nchi katika kipindi husika, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 71.4 ya pato la taifa kwa mwaka 2018. Fedha hizo zilizotoroshwa kutoka Tanzania ni nyingi kuliko fedha ambazo Tanzania ilikopa katika kipindi hicho cha miongo mitano, ambazo ni dola za Marekani bilioni 18.6. Utafiti huu unadhihirisha kuwa, iwapo Afrika itadhibiti uhamishaji na utoroshaji wa fedha basi haitakuwa na haja ya kutegemea mikopo ya nje.

**(vi) Aina ya Uwekezaji**

Kuna changamoto kubwa katika kutafsiri maana ya uwekezaji unaopewa ulinzi na MIUMBI ingawa kwa ujumla dhana ya uwekezaji inalenga mtaji, fedha na mali zote zinazoingizwa katika nchi. MIUMBI iliyo mingi haiweki bayana aina ya uwekezaji unaolindwa na viwango au vigezo vya uwekezaji na hivyo hupelekea migogoro ya kisheria. Baadhi ya MIUMBI imetaja kuwa uwekezaji ni vitu au mali inayotumika tu kwa ajili ya uzalishaji faida moja kwa moja ili kuondoa utata wa tafsiri.

Kwa jumla, kuna aina tatu za ulinzi wa uwekezaji katika MIUMBI. Aina ya kwanza ni ulinzi wa mtaji au mali inayohamishika na iliyovuka mipaka kwa ajili ya uzalishaji (*asset-based model)*. Aina ya pili ni ulinzi wa mali–fedha (*capital*) pekee na siyo mali inayomilikiwa na mwekezaji. Aina ya tatu ni ulinzi wa mfumo wa uzalishaji kama kampuni au kiwanda (*enterprise-based*).

Kuwa na tafsiri ya wazi kuhusu aina na vigezo vya uwekezaji kunasaidia sana katika utetezi pale unapoibuka mgogoro kati ya mwekezaji na serikali. Tafsiri hiyo ya wazi ya uwekezaji ndiyo itakayotumika kupima ukubwa wa athari ambazo mwekezaji anasemekana kuzipata kutokana na hatua zinazochukuliwa na serikali.

Nchi nyingi za Kusini, ikiwemo Tanzania, huingia MIUMBI inayotoa tafsiri ya jumla ya uwekezaji na mwekezaji. Kwa tafsiri hiyo pana, uwekezaji humaanisha "aina zote za mali" zilizowekezwa kutoka nchi inayosafirisha mtaji katika nchi inayopokea mtaji kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi hiyo. Tafsiri hii inaweza ikatumika kumaanisha fedha, teknolojia, magari, mkopo, hisa, mtaji–kauli au mfumo wowote wa amana. Kwa maana hiyo, serikali inaweza ikashitakiwa na kampuni nyingine iliyoingia mkataba na kampuni iliyowekeza ndani ya nchi au kampuni tanzu kwa kisingizio cha kupoteza faida tarajiwa (*indirect controlled asset*). Tanzania, kwa mfano, imeshawahi kushitakiwa na benki iliyotoa fedha kwa ajili ya uwekezaji ingawa benki hiyo haikuwa sehemu ya mkataba au wawekezaji wa moja kwa moja. Kesi hiyo, iliyofunguliwa na benki ya Standard Chartered ya Hong Kong (SCB–HK) katika mahakama ya ICSID, ilitolewa hukumu mwezi Oktoba 2019 ambapo Tanzania iliamriwa kuilipa benki hiyo kiasi cha dola za Marekani milioni 185.45 sawa na shilingi bilioni 432.7[10].

[10] *The EastAfrican,* "World Bank Court Orders Tanzania to Pay $185 Million to Standard Chartered," Oktoba 16, 2019. Imepatikana Oktoba 25, 2020 kutoka https://www.theeastafrican.co.ke/tea/business/world-bank-court-orders-tanzania-pay-185-million-to-standard-chartered-1429424

**(vii) Muda na Ukomo wa Mkataba**

Kwa kawaida, MIUMBI hutoa muda maalum wa uhai wake ikiwemo tarehe ya kuanzia na tarehe ya ukomo wake. Maana yake ni kuwa pande mbili ziwe tayari kutimiza wajibu wao ndani ya muda husika. Sehemu kubwa ya MIUMBI huwa na uhai wa kati ya miaka 10 hadi 15 tangu siku iliporidhiwa na mamlaka husika baada ya kutiwa sahihi. Ipo pia baadhi ya MIUMBI isiyokuwa na ukomo kwa maana ya kuwa huendelea kuwa hai hadi pale nchi zilizoingia mkataba zitakapoamua kwa hiari yao kusitisha makubaliano hayo. Mfano wa MIUMBI isiyo na ukomo ni mkataba kati ya Korea na Thailand wa mwaka 2002.

MIUMBI huwa na vifungu vinavyoweka taratibu za kuendeleza, kusitisha au kujadili upya mkataba pale ambapo mkataba husika utakuwa umefikia ukomo. Hii inaweza kufanyika kwa njia ya kutoa taarifa au notisi ya kurudi mezani kwa ajili ya majadiliano mapya kabla ya mkataba wa awali kufutwa. Pande mbili zinaweza kuamua kwa hiari kutojadili upya mikataba husika au kukaa kimya na kuendelea na utaratibu wa awali kana kwamba wamehuisha mkataba husika.

Ifahamike kuwa baada ya kuridhiwa na kuanza kutumika, MIUMBI hulinda uwekezaji wote kutoka nchi mbia, ukiwemo uwekezaji uliofanyika kabla ya mkataba husika haujaingiwa. Pia, iwapo mojawapo ya nchi ambayo ni mbia wa mkataba isipotoa maandishi ya kujiondoa kwa wakati basi mkataba huo wa MIUMBI uliofikia ukomo hujihuisha wenyewe kwa

kipindi kingine cha miaka 10 au 15. Vilevile, hata baada ya MIUMBI kufikia ukomo, na nchi ya Kusini ikaamua kujiondoa kwa kufuata taratibu za kisheria bado uwekezaji uliofanyika kwenye nchi hiyo ya Kusini huendelea kulindwa na mkataba husika kwa kipindi kingine cha miaka 15.

**(viii) Vibali vya Kazi na Utaalamu**

MIUMBI mingi hutoa ulinzi kwa wawekezaji pamoja na wafanyakazi wa kigeni ikielezea taratibu za kupatikana kwa vibali vya kazi. Inaweza kuainisha idadi ya wafanyakazi wa kigeni, nafasi na kiwango cha weledi unaohitajika katika kusimamia uwekezaji. Taratibu za uhamiaji na ajira hutakiwa kutoa upendeleo kwa wafanyakazi wa kigeni walioainishwa kama sehemu ya kuhamasisha uwekezaji.

Kwa kulinda haki ya wawekezaji kutumia wafanyakazi wa kigeni, MIUMBI huzuia nchi za Kusini kulinda ajira kwa ajili ya raia wake kama sehemu ya kukuza weledi na utaalamu wa ndani. Nchi za Kusini huvutia uwekezaji kwa lengo la kuongeza ajira zitakazosaidia kuwatoa wananchi wake kwenye lindi la umaskini. Nchi hizi zinapozuiwa kuweka mikakati ya kuongeza idadi ya ajira, na hasa ajira zenye staha kwa wananchi wao, hujikuta kwenye misukosuko ya kisiasa na kiuchumi. Azima ya kuhakikisha wananchi wanamiliki angalau sehemu ya uchumi haiwezi kutimia iwapo MIUMBI inalinda ajira za wageni. Nchi na raia wake watabakia kuwa watazamaji huku wageni wakivuna utajiri na kubakiza umaskini.

# SURA YA 4

# UTATUZI WA MIGOGORO YA UWEKEZAJI

Historia inatuelezea kuwa wakati nchi za Magharibi zilipokuwa zikipigania makoloni ili kupora rasilimali za Afrika, migogoro mingi iliibuka baina yao. Nchi hizo za Magharibi zilikuwa zikitumia nguvu za kijeshi (*gun boat diplomacy*) kumaliza migogoro hiyo. Maana yake ni kuwa nguvu ya kijeshi ndio ilionekana kuwa njia ya pekee ya kulinda 'uwekezaji' na maslahi ya kibiashara baina ya nchi zilizokuwa na nguvu za kiuchumi duniani.

Baada ya vita vya pili vya dunia, nchi za Magharibi ziliona umuhimu wa kuandaa mfumo wa kisheria wa utatuzi wa migogoro ili kuepuka vita. Makubaliano yalifanyika baina ya wababe wa vita ili waendelee kufaidi rasilimali kutoka kwenye makoloni bila kupigana wao kwa wao. Na huo ndio ukawa mwanzo wa mifumo ya kimataifa ya utatuzi wa migorogo ya kibiashara ambayo imo katika MIUMBI. Kwa kutumia mifumo hii, mwekezaji kutoka moja ya nchi zilizosaini MIUMBI anaweza kuishitaki serikali ya nchi ya pili kwa kukiuka masharti au kipengele chochote cha mkataba husika.

Ni mara chache sana ambapo serikali za nchi za Kusini zimewahi kushitaki kampuni kwa kutumia MIUMBI au hata kushinda kesi. Kimsingi MIUMBI inalenga kulinda maslahi ya kibiashara ya wawekezaji na nchi wanazotoka.

Kuna mifumo kadhaa ya utatuzi wa migogoro inayohusu uwekezaji na ni wajibu wa pande mbili kuamua ni mfumo upi utafuatwa pindi unapoibuka mgogoro kati yao. Maelezo juu ya mifumo husika huwekwa ndani ya MIUMBI. Kati ya mifumo hiyo ya usuluhishi, mifumo miwili ndiyo hutumika zaidi. Wa kwanza ni *International Centre on the Settlement of Investment Disputes* (*ICSID*) *Convention and Rules of Arbitration* ambao upo chini ya Benki ya Dunia. Mfumo mwingine ni *The United Nations Commission on International Trade Law (UNCITRAL) Rules* ambao upo chini ya Umoja wa Mataifa.

Muundo wa jopo la usuluhishi na utatuzi wa migogoro kati ya nchi na mwekezaji unafanana na ule wa utatuzi wa migogoro ya kibiashara (*commercial arbitration*) inayohusisha watu binafsi. Mashauri husikilizwa na wasuluhishi watatu, ambapo kila upande huteua msuluhishi mmoja. Baada ya hapo, pande zote mbili hukubaliana na kumteua mwenyekiti wa jopo la wasuluhishi. Kigezo kikubwa kinachotumika, mbali na umahiri wa sheria za kibiashara, ni kuaminika na kutokupendelea upande wowote. Taratibu za kuendesha mashauri hukubaliwa na pande zote mbili kabla ya kuanza kusikilizwa kwa malalamiko. Taratibu hizo hufuata miongozo ya usuluhishi inayotumika chini ya makubaliano mbalimbali ya kimataifa.

Mikataba mingi ya uwekezaji hutoa fursa ya hadi miezi sita kwa mwekezaji na nchi husika kukutana na kukubaliana jinsi ya kutatua mgogoro wao. Katika kipindi hicho, mlalamikaji hutoa notisi kwa upande anaoulalamikia kuhusu azima yake ya kufungua shauri mahakamani au katika kituo cha usuluhishi kama hakutakuwa na mapatano ya hiari baina yao. Pale inaposhindikana au upande mmoja kupuuzia ndipo malalamiko huwasilishwa kwenye mifumo ya kimataifa ya kimahakama kwa ajili ya usuluhishi.

**Mifumo ya Usuluhishi Duniani**

Kuna vituo na mifumo mbalimbali ya kimataifa ya usuluhishi wa migogoro ya biashara na uwekezaji duniani. Baadhi imeainishwa hapa chini.

(i) *International Centre for Settlement of Investment Disputes (ICSID)*

Hii ni taasisi ya kimataifa ya usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji iliyoundwa mwaka 1966 chini ya Benki ya Dunia kwa lengo la kulinda uwekezaji dhidi ya maamuzi ya kisiasa au hatari zisizo za kibiashara. Takribani nchi 153 duniani kote zimeridhia taratibu na mfumo wa taasisi hii.

(ii) *The United Nations Commission on International Trade Law (UNCITRAL)*

Taasisi hii iliundwa na Umoja wa Taifa mwaka 1966 kwa lengo la kuhuisha na kuwianisha sheria za kimataifa zinazohusu masuala ya biashara na uwekezaji. Taasisi hii huandaa na kuhuisha taratibu na kanuni za utatuzi wa migogoro ya biashara lakini yenyewe haijishughulishi na utatuzi wa

migogoro hiyo.

(iii) *The Arbitration Institute of the Stockholm Chamber of Commerce (SCC)*
Taasisi hii, iliyoundwa mwaka 1917 kama sehemu ya Chama cha Wafanyabiashara cha Stockholm (Stockholm Chamber of Commerce), inatoa huduma kwa wawekezaji wenye asili ya Kiswidi pamoja na wengine duniani wanaotaka jukwaa huru kwa ajili ya kusuluhisha migogoro ya kibiashara. Mwaka 1977 ilipata umaarufu baada ya kukubaliwa kutatua migogoro kati ya Urusi na Marekani katika kipindi ambacho nchi hizo zilikuwa katika vita baridi vya kisiasa na kiuchumi.

(iv) *The ICSID Additional Facility*
Taasisi hii iliundwa mwaka 1978 kwa ajili ya usuluhishi wa migogoro ya kibiashara na uwekezaji kwa wale ambao hawajaridhia mikataba ya awali ya ICSID. Taasisi hii hutumika zaidi wakati upande mmoja katika mkataba ni mwanachama wa ICSID na upande wa pili ukiwa siyo mwanachama.

Mbali na taasisi za kimataifa za usuluhishi zilizojadiliwa hapo juu, zipo zingine kama Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya London (*London Court of International Arbitration)*, Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi cha Dubai (*Dubai International Arbitration Centre*), Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi cha Vienna (*Vienna International Arbitration Centre*), Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi cha Singapore (*Singapore International Arbitration Centre*) na Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro ya Biashara (*International Court of Arbitration* –

*ICA*).

**Changamoto katika Utatuzi wa Kimataifa wa Migogoro ya Uwekezaji**

Kumekuwa na mapungufu kadhaa kuhusu matumizi ya mahakama za kimataifa kwenye migogoro ya uwekezaji na biashara. Baadhi ya mapungufu hayo yamejadiliwa hapa chini.

(i) *Kukosekana kwa Uhalali wa Wasuluhishi*

Jopo la watu watatu huteuliwa kufanya maamuzi kuhusu mgogoro kati ya mwekezaji na nchi. Watu hawa watatu wanakuwa na nguvu ya kufanya maamuzi makubwa yanayoweza kuathiri maslahi mapana ya nchi huru. Pia, imeonekana kuwa wasuluhishi huteuliwa kutokana na orodha ya wataalamu inayotolewa chini ya mfumo husika wa utatuzi. Wengi wao ni washiriki, kwa njia moja au nyingine, katika kulinda maslahi ya kibiashara ya wawekezaji. Kwa mfano, utakuta mmoja wa wasuluhishi ameshiriki kama mwanasheria wa kampuni ya Kimagharibi katika majadiliano ya mkataba kati ya kampuni hiyo na nchi ya Kusini. Kisha unapotokea mgogoro kati ya kampuni hiyo na nchi ya Kusini, kampuni hiyo inamteua mwanasheria huyo huyo kuwa 'jaji'. Hii inaleta mgongano wa maslahi unaolalamikiwa na nchi nyingi za Kusini ambazo zimeshiriki kwenye mashauri haya. Pia, wawekezaji hupewa ulinzi wa kidiplomasia na nchi zao, jambo linalowapa nguvu kubwa katika mfumo wa kimataifa wa utatuzi wa migogoro. Hii inaufanya upande wa pili, kwa maana ya nchi ya Kusini inayopokea uwekezaji, kutoweza kulinda ipasavyo maslahi yake.

(ii) *Kukosekana kwa Uwazi*
Mchakato wa uendeshaji na usikilizaji wa migogoro hauwekwi wazi kwa umma. Taarifa na maelezo ya kesi haitolewei kwa mtu mwingine hadi pale uamuzi wa mwisho utakapotolewa. Hali hii inawakosesha wananchi au wadau wengine wataoathirika na maamuzi hayo fursa ya kufuatilia mwendendo wa kesi au kuwasilisha hoja zao ipasavyo.

(iii) *Hiari ya Kuchagua Utaifa*
Wawekezaji wanaweza kupata nafasi ya kuishitaki nchi walimowekeza kwa kupitia mgongo wa kampuni tanzu inayotoka kwenye nchi ya tatu iliyoingia MIUMBI na nchi walimowekeza. Tuchukulie, kwa mfano, kampuni yenye asili yake nchini Malaysia ambayo imewekeza nchini Tanzania lakini ina wanahisa kutoka Uingereza au hupokea fedha kutoka benki ya Uingereza. Iwapo patatokea mgogoro kati ya kampuni husika na Tanzania basi kampuni hiyo inaweza kutumia MIUMBI kati ya Uingereza na Tanzania kuishitaki Tanzania alimradi kampuni hiyo iweze kuonyesha jinsi wawekezaji wake wa Uingereza walivyoathirika kibiashara na maamuzi yaliyofanywa na Tanzania.

Mfano uliotolewa hapo juu siyo wa kufikirika kwani kisa kama hicho kimeshawahi kuikumba Tanzania. Kwenye jedwali la kesi zilizofunguliwa dhidi ya Tanzania lililoonyeshwa katika sura ya 5, ipo pia kesi ya benki ya FBME dhidi ya Tanzania iliyofunguliwa mwaka 2019. Benki ya FBME iliwahi kugundulika kujihusisha na utakatishaji wa fedha na hivyo kupelekea serikali ya nchi ya Cyprus kuifungia nchini humo.

Tanzania ilipochukua hatua kama hiyo, mmiliki wa FBME, Ayoub–Farid Michael Saab, akaifungulia mashitaka kwenye mahakama ya ICSID iliyoko chini ya Benki ya Dunia. Saab ni raia wa Lebanon ambayo haina MIUMBI na Tanzania. Ili aweze kuishitaki Tanzania, Saab akaamua kuchukua uraia wa nchi ya Uholanzi na hivyo kutumia MIUMBI kati ya Uholanzi na Tanzania kuishitaki Tanzania[11]. Japokuwa Tanzania ilisitisha MIUMBI kati yake na Uholanzi Aprili 2019, bado mkataba huo unaendelea kutoa ulinzi wa miaka 15 kwa uwekezaji wote uliofanyika kabla ya kusitishwa kwake.

(iv) *Kukosekana kwa Mamlaka ya Rufaa*

Maamuzi yanayotolewa na mahakama za kimataifa za usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji hayana vipengele vya rufaa. Pia, hakuna utaratibu wa pingamizi ili kuwaondoa wajumbe wa kamati hiyo ya usuluhishi iwapo watagundulika wana maslahi.

(v) *Mzigo wa Gharama za Kesi na Fidia*

Mara nyingi mahakama za kimataifa huketi nje ya nchi na ni gharama kubwa sana kwa nchi zinazoendelea. Wakili wa kimataifa hulipwa kiasi cha dola za Marekani 1,000 (sawa na Sh. 2,300,000/=) kwa saa kuiwakilisha nchi katika mahakama za kimataifa za usuluhishi wa migogoro. Kampuni za uwekezaji zimekuwa zikimudu kwa kuajiri mawakili hodari kwa gharama kubwa kutokana na kuwa na uhakika wa

[11]Emmanuel K. Mwesiga, "White–Collar Crimes: The Rise and Fall of FBME Bank Tanzania," *The Chanzo Initiative,* Machi 14, 2022. Imepatikana Juni 28, 2022 kutoka https://thechanzo.

kushinda mashauri haya. Mashauri ya migogoro ya uwekezaji huchukua hadi miaka mitatu kukamilika kutegemeana na uzito wa hoja na utayari wa pande zinazoshitakiana. Kwa jumla, hadi shauri limalizike nchi hulipa wastani wa dola za Marekani milioni 8 (sawa na Sh. bilioni 18.7) zikiwa ni gharama za wasuluhishi, malipo ya mawakili na maafisa wanaohusika pamoja na usafiri na malazi. Kwa baadhi ya mashauri, gharama hupaa hadi dola za Marekani milioni 30 (takribani Sh. bilioni 70)[12].

Mzigo mwingine wa gharama kwa nchi za Kusini hutokana na fidia ambazo mahakama huamuru nchi za Kusini zilipe kwa kampuni za uwekezaji, pale ambapo kampuni hizo hushinda kesi. Mabilioni ya fedha, ambayo yangeweza kwenda katika huduma za kijamii au miradi ya maendeleo, hulipwa kwa kampuni hizo za kimataifa kama fidia. Kwa mfano, "[m]waka 2012, mahakama ya uwekezaji iliiamuru nchi ya Ecuador kuilipa kampuni ya Kimarekani, Occidental Petroleum, kiasi cha dola bilioni 1.77 (takribani Sh. trilioni 4.13) kwa kufuta mkataba wa uchimbaji mafuta. Ukiongezea na riba na gharama za kesi, Ecuador itatakiwa kuilipa kampuni hiyo dola bilioni 2.4 (takribani Sh. trilioni 5.6)."[13] Kiasi hicho kingetosha kugharamia huduma za afya kwa watu wote milioni 7 wa taifa hilo kwa mwaka huo wa 2012. Nchi inaposhindwa kwenye kesi kama hii inaongezea mzigo

com/2022/03/14/white-collar-crimes-the-rise-and-fall-of-fbme-bank-tanzania/

[12]Burghard Ilge, "To Change a BIT Is Not Enough: On the Need to Create Sound Policy Frameworks for Investment" (Utrecht: Both ENDS, 2015), uk. 7.

[13]Kama hapo juu, uk. 7.

wa madeni na kudhoofisha uchumi zaidi hivyo kuathiri maendeleo. Mashauri yanayofunguliwa katika mahakama hizo ni kikwazo kwa nchi za Kusini kuleta ustawi kwa watu wake na kuendeleza uchumi wake.

**Mbadala wa Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji Nje ya Nchi**

Yapo mapendekezo mbalimbali ambayo yametolewa ili kujenga mbadala wa mifumo ya kimataifa ya utatuzi wa migogoro baina ya wawekezaji toka ughaibuni na serikali za nchi za Kusini. Baadhi ya mapendekezo hayo yamejadiliwa hapa chini:

(i) *Kuimarisha Mifumo ya Ndani ya Utoaji Haki*

Mojawapo ya visingizio vinavyotolewa na wawekezaji kwa wao kukimbilia katika mahakama za kimataifa ni kutokuwa na imani na mifumo ya utoaji haki ya ndani ya nchi. Wawekezaji wengi hudai kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya mhimili wa utawala na ule wa mahakama hali inayopelekea maamuzi ya mhimili wa utawala kuamua mwenendo wa mashauri ya mahakama. Japo ina ukweli ndani yake, hoja hii hutolewa kama kisingizio tu kwa sababu, kwa sehemu kubwa, katika mfumo wa soko huria, madola ya nchi za Kusini hutumikia wawekezaji wa kutoka ughaibuni ambao maslahi yao yamelindwa na sera, sheria na mikataba mbalimbali. Kama ilivyojadiliwa katika vipengele vilivyotangulia, mifumo ya kimataifa ya usuluhishi wa migogoro iliwekwa mahususi kwa ajili ya kulinda maslahi ya wawekezaji, na kwa maana hiyo kunapotokea mgogoro kati ya serikali ya Kusini na

mwekezaji ni maslahi ya mwekezaji ndiyo yameonekana kupewa kipaumbele.

Hoja ya udhaifu wa mifumo ya ndani ya utoaji haki inapaswa kujibiwa kwa nchi za Kusini kuimarisha mifumo ya ndani ya utoaji haki ili kuhakikisha kuwa mahakama za nchi za Kusini zinakuwa vyombo huru vya utoaji haki bila kuingiliwa na mhimili wa utawala. Mageuzi ya kutenganisha mihimili ya dola yanapaswa kufanyika kwa maslahi mapana ya utoaji haki kwa wote na siyo tu kwa ajili ya kutimiza matakwa ya wawekezaji. Ni vema zifanyike juhudi za dhati kutenga rasilimali fedha kugharamia miundombinu na vitendea kazi na kuongeza na kuendeleza rasilimali watu kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa ndani wa utatuzi migogoro ya kibiashara.

(ii) *Makubaliano Nje ya Mahakama*

Makubaliano nje ya mahakama hutoa fursa kwa pande mbili zenye mgogoro kukubaliana kuhusu changamoto zilizoibuka au gharama wanazodaiana. Hii inaondoa haja ya kuingia kwenye utaratibu mrefu na wa gharama kubwa za uendeshaji kesi katika mahakama za kimataifa. Hata hivyo, kampuni nyingi za uwekezaji zinapoanzisha mgogoro hutoa madai makubwa ya fidia au kuingilia uhuru wa ndani wa kutunga sera na sheria na hivyo kupelekea makubaliano nje ya mahakama kuwa mwiba kwa nchi za Kusini.

(iii) *Vituo Mbadala vya Utatuzi wa Migogoro Afrika*

Vipo baadhi ya vituo vya usuluhishi kama *Kigali International Arbitration Center* (KIAC), *Nairobi Centre for International*

*Arbitration* ambavyo vimeanzishwa barani Afrika kwa lengo la kupunguza gharama na muda unaotumika kuendesha mashauri nje ya bara la Afrika. Tanzania pia imo katika mchakato wa kuanzisha *Tanzania Arbitration Centre*. Hata hivyo, gharama kubwa sana huhitajika katika kuendesha vituo hivi. Pia, kama ambavyo hawaamini mifumo ya ndani ya utoaji haki, wawekezaji wengi pia hawaamini kuwa vituo hivi vina uhuru na umahiri wa kusuluhisha migogoro ya uwekezaji.

**Hitimisho**

Sura hii imechambua mifumo mbalimbali ya kimataifa ya usuluhishi wa migogoro iliyoanzishwa kwa ajili ya kusuluhisha migogoro kati ya wawekezaji na serikali. Changamoto zinazojitokeza katika mifumo hii pia zimejadiliwa, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa uhalali wa wasuluhishi, kukosekana kwa uwazi katika mwenendo wa mashauri, hiari ya kampuni za uwekezaji kuchagua utaifa, kukosekana kwa mamlaka ya rufaa na mzigo mkubwa wa gharama za kesi na fidia.

Njia tatu zimetolewa kama mbadala wa mifumo ya kimataifa. Katika hizi tatu, njia ambayo itatoa mbadala halisi ni kuimarisha na kutumia mifumo ya utoaji haki ya ndani ya nchi, mahakama na sheria za ndani, kwa ajili ya utatuzi wa migogoro kati ya wawekezaji na serikali. Njia mbadala zingine mbili, yaani makubaliano nje ya mahakama na vituo mbadala vya utatuzi wa migogoro Afrika, zinaweza tu kupunguza ukubwa wa tatizo lakini haziwezi kuliondoa

kabisa. Njia hizi mbili zikifanyiwa kazi zinaweza kupunguza ukubwa wa gharama ambazo serikali za Kusini hutozwa pale zinaposhindwa katika mashauri yaliyosuluhishwa kwenye mahakama za kimataifa. Kamwe njia mbadala hizi haziwezi kuondoa kisababishi kinachozichochea kampuni za ughaibuni kuziburuza nchi za Kusini mahakamani. Na kisababishi hicho, kama ilivyojadiliwa tangu mwanzo wa kitabu hiki, ni sheria na mikataba ya kimataifa, ikiwemo MIUMBI, ambayo hutoa upendeleo mkubwa kwa kampuni za ughaibuni kwa gharama ya nchi za Kusini.

# SURA YA 5

# MIUMBI ILIYOINGIWA NA TANZANIA NA ATHARI ZAKE

Taarifa zilizopo kwenye tovuti ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Biashara na Maendeleo Duniani (UNCTAD) zinaonyesha kuwa hadi mwaka 2022 kulikuwa na MIUMBI kumi na tisa (19) kati ya Tanzania na nchi zingine ambayo ilikuwa katika utekelezaji[14]. Nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini (2005), Canada (2013), China (2013), Denmark (1999), Italia (2001), Korea (1998), Kuwait (2013), Mauritius (2009), Misri (1997), Omani (2012), Uswidi (1999), Ufini (2001), Uholanzi (2001), Uingereza (1994), Ujerumani (1965), Uswisi (2004), Uturuki (2011), Yordani (2009), na Zimbabwe (2003). Tarehe 1 Oktoba 2018, Tanzania iliwasilisha notisi ya kujiondoa kwenye mkataba na Uholanzi, ambao ulikuwa ulikuwa unafikia ukomo Aprili 1, 2019. Hata hivyo, mkataba huu utaendelea kutoa ulinzi wa miaka 15 kwa uwekezaji wote toka Uholanzi uliofanyika kabla ya Aprili 1, 2019.

[14]"International Investment Agreements Navigator: United Republic of Tanzania–Bilateral Investment Treaties," UNCTAD. Imepatikana Juni 30, 2022 kutoka https://investmentpolicy.unctad.org/international-investment-agreements/countries/222/tanzania-united-republic-of

MIUMBI yote iliyoorodheshwa hapo juu ina vipengele vinavyofafana vyenye lengo la kutoa ulinzi kamili kwa wawekezaji kutoka nchi zilizoko kwenye mkataba. Licha ya ufanano huo mkubwa, zipo tofauti chache ndogo ndogo. Mathalani, mkataba wa MIUMBI kati ya Ujerumani na Tanzania hauna kipengele kinacholazimisha mashitaka yapelekwe kwenye mahakama za kimataifa. Sababu ya kukosekana kwa kipengele hicho ni kuwa mkataba huo ulisainiwa mwaka 1965 na wakati huo sehemu kubwa ya mifumo ya usuluhishi ya kimataifa inayotumika hivi sasa haikuwepo. Mkataba wa MIUMBI kati ya China na Tanzania unaitambua mifumo ya usuluhishi ya ndani ya nchi sambamba na ile ya kimataifa na unawahimiza wawekezaji watakaokuwa na mgogoro na nchi walimowekeza kutumia kwanza mifumo ya ndani ya utatuzi wa migogoro kabla ya kwenda kwenye ile ya kimataifa.

Ifahamike kuwa hata pale ambapo MIUMBI haitaji kutumika kwa mifumo ya kimataifa (kama katika mkataba wa MIUMBI kati ya Ujerumani na Tanzania), bado Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania ya 1997 (kifungu cha 23(2)(b)) inatoa fursa kwa wawekezaji kufungua mashitaka kwenye Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migorogo ya Uwekezaji (ICSID)[15]. Pia, ipo baadhi ya mikataba kati ya kampuni ya uwekezaji na serikali ambayo ina vipengele vinavyoruhusu matumizi ya mifumo ya kimataifa ya utatuzi wa migogoro. Vipengele hivi huwekwa kuhakikisha kuwa Tanzania haiwezi kubadilisha mikataba

[15]Soma fungu la 23(2)(b) la *Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania, 1997.*

hii hata kama ni mikataba ya kinyonyaji inayoigharimu nchi. Kadhalika, hata pale nchi inapoamua kubadili sera na sheria zake ili kukomesha uporaji wa rasilimali zake, mikataba ya kampuni na serikali pamoja na ile ya MIUMBI huwa ni kikwazo kwa mabadiliko hayo kwani kampuni huitumia ili kuishitaki nchi. Hili limewahi kuikumba Tanzania.

Mwaka 2017, Tanzania ilitunga sheria kadhaa kwenye sekta ya mafuta na madini ili kuongeza manufaa kwa taifa na wananchi. Sheria hizi zilikuja kwa ajili ya kujibu malalamiko ya muda mrefu ya wananchi na asasi za kiraia kuhusu kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa sekta ya madini na mafuta kulikopelekea upotevu wa mapato, uharibifu wa mazingira na ukiukwaji wa haki za binadamu[16]. Mojawapo ya sheria zilizopitishwa ni ile iliyoweka mamlaka ya kudumu ya dola juu ya rasilimali na utajiri asilia uliomo nchini Tanzania inayojulikana kama *Natural Wealth and Resources* (*Permanent Sovereignty*) Act, 2017. Pia, kupitia sheria ya mabadiliko ya sheria mbalimbali ya mwaka 2017, ijulikanayo kwa Kiingereza kama *Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017*, Tanzania ilifanya marekebisho ya *Sheria ya Madini ya 2010* ili kuondoa vifungu vilivyokuwa vinaizuia Tanzania kufaidika na uchimbaji wa madini. Sheria nyingine iliyopitishwa ni ile iliyoipatia Tanzania mamlaka ya kubatilisha mikataba yote isiyokuwa na tija au manufaa kwa nchi na wananchi, ambayo

[16]Mark Curtis na Wenzake, *The One Billion Dollar Question: How Can Tanzania Stop Losing So Much Tax Revenue* (Dar es Salaam: TEC, BAKWATA na CCT, 2012).

kwa Kiingereza inajulikana kama *Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*. Sheria hizi zina vipengele vingi ila vipengele vitano (5) ndivyo vyenye uzito zaidi[17]. Maudhui ya vipengele hivyo ni:
(i) Tanzania kama nchi huru inayo mamlaka ya kudumu (*permanent sovereignty*) juu ya utajiri asilia na rasilimali zake.
(ii) Katika kila mradi mkubwa wa uchimbaji wa madini, serikali ya Tanzania itapata hisa zisipopungua asilimia 16 ambazo zitatolewa bure. Kadhalika, Serikali ina haki ya kutwaa hadi asilimia 50 ya hisa katika kampuni iliyowekeza katika madini.
(iii) Migogoro kati ya wawekezaji na serikali itatuliwe kwa kutumia sheria za ndani na vyombo vya kisheria vya Tanzania.
(iv) Uchakataji wa madini ufanyike nchini.
(vi) Bunge na Serikali vinayo mamlaka ya kupitia upya mikataba ya uwekezaji katika sekta ya madini na mafuta ili kurekebisha vifungu vinavyoinyonya Tanzania.

Wawekezaji kutoka ughaibuni waliowekeza katika sekta za madini na mafuta pamoja na viongozi wa nchi za Magharibi waligoma kuzitambua sheria zilizotajwa hapo juu wakidai zimelenga kutaifisha migodi na kuleta hasara kwa wawekezaji. Baadhi waliamua kuipeleka Tanzania katika mahakama za kimataifa kudai fidia wakitumia mwanya wa MIUMBI.
Mwaka 2020, kampuni tatu za madini, zikiwemo Indiana Resources ya Australia, Winshear Gold Corp na Montero Mining and Exploration Ltd za nchini Canada zilifungua kesi

[17]Sabatho Nyamsenda, "Bulldozing like a Fascist? Authoritarian Populism and Rural Activism in Tanzania," Emancipatory Rural Politics Initiative (ERPI) Conference, The Hague, Machi 17-18, 2018.

katika mahakama ya ICSID kudai fidia zikidai kuathiriwa na mabadiliko yaliyofanywa na Tanzania kupitia sheria mpya za madini. Kampuni ya Indiana Resources inaidai Tanzania fidia ya dola za Marekani milioni 93.7 (sawa na Sh. bilioni 218.5), pamoja na riba ambayo inazidi kuongezeka kila uchao[18] . Kiasi cha fidia ambacho Indiana Resources inataka kulipwa ni kikubwa kuliko mtaji wa kampuni hiyo ambao unakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 17.8 (sawa na Sh. bilioni 41.5)[19].

Indiana Resources ni kampuni ya nchini Australia lakini ina kampuni tanzu zilizosajiliwa Uingereza na hivyo inatumia mkataba wa MIUMBI kati ya Uingereza na Tanzania kuishitaki Tanzania. Kampuni ya Litigation Capital Management Limited (LCM) imetoa dola za Marekani milioni 4.7 (sawa na Sh bilioni 10.96) kwa ajili ya kugharamia kesi ya Indiana ilhali kampuni ya Omni Bridgeway Canada Limited imetoa dola za Marekani milioni 2.32 (sawa na Sh bilioni 5.4) kwa ajili ya kugharamia kesi ya Montero Mining and Exploration Ltd. Kampuni hizo zilizolipia gharama za kesi zinatarajia kurudisha gharama hizo pamoja na faida kwani zina uhakika kuwa kampuni za Indiana na Montero zitashinda kesi na Tanzania itaamriwa kulipa fidia pamoja na gharama za kuendeshea kesi husika. Tukionacho hapa ni kujengeka kwa "mtandao wa kampuni za kibepari za

[18]Indiana Resources Limited, "Update on ICSID Arbitration – Republic of Tanzania," Januari 2022. Imepatikana Juni 25, 2022 kutoka https://indianaresources.com.au/wp-content/uploads/2022/01/20210124-IDA-Update-on-ICSID-Arbitration-Republic-of-Tanzania.pdf

[19]*Stockhead,* "Indiana Optimistic of Tanzanian Nickel Resolution After Government Meetings," 12 Aprili 2022. Imepatikana Juni 25, 2022 kutoka https://stockhead.com.au/resources/indiana-optimistic-of-tanzanian-nickel-resolution-after-government-meetings/

kimataifa zinazounganisha nguvu dhidi ya Tanzania na zina uhakika wa kuibuka na ushindi''[20]

[20]Sabatho Nyamsenda, "Watanzania Kizimbani: Jinsi Kampuni za Madini Zilivyojipanga Kuiangamiza Tanzania," *Udadisi: Rethinking in Action,* Septemba 15, 2020. Imepatikana Juni 25, 2022 kutoka https://udadisi.com/watanzania-kizimbani-jinsi-kampuni-za/

**Jedwali 1: Mashauri Yaliyofunguliwa na Kampuni za Nje dhidi ya Tanzania katika Kituo cha ICSID**

| | Jina la Kampuni[21] | Fidia Inayodaiwa | Mkataba Unaotumika | Uamuzi wa Mahakama |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Montero Mining and Exploration Ltd (ICSID Case No. ARB/21/6) | | MIUMBI kati ya Canada na TZ | Kesi inaendelea |
| **2.** | Indiana Resources Ltd kupitia kampuni tanzu za Nachingwea U.K. Ltd, Ntaka Nickel Holding Ltd & Nachingwea Nickel Ltd. (ICSID Case No. ARB/20/38) | Sh. bilioni 218.3 | MIUMBI kati ya Uingereza na TZ | Kesi inaendelea |
| **3.** | Winshear Gold Corp (ICSID Case No. ARB/20/25) | Sh. bilioni 223.8 | MIUMBI kati ya Canada na TZ | Kesi inaendelea |
| **4.** | Symbion Power Tanzania Ltd & wengine (ICSID Case No. ARB/19/17) | Sh. trilioni 3.7 ($1.57bln) | MIUMBI kati ya Uingereza na TZ | Kesi iliondolewa mahakamani Mei 2021 baada ya pande zinazoshitakiana kukubaliana kumaliza mgogoro nje ya mahakama |
| **5.** | Benki ya FBME kupitia mmiliki wake, Ayoub-Farid Michael Saab (ICSID Case No. ARB/19/8) | | MIUMBI kati ya Uholanzi na TZ | Kesi iliondolewa mahakamani Juni 2021 baada ya pande zinazoshitakiana kukubaliana kumalizana nje ya mahakama |

[21]Kwenye kila namba ya kesi, namba iliyo katikati huwakilisha mwaka ambamo kesi husika ilifunguliwa. Kwa mfano, katika ICSID Case No. ARB/21/6, namba 21 inawakilisha mwaka 2021 na huo ndio mwaka ambamo kesi husika ilifunguliwa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **6.** | EcoDevelopment in Europe AB & Eco-Energy Africa AB (ICSID Case No. ARB/17/33) | Sh. trilioni 1.2 ($500mln) | MIUMBI kati ya Sweden na TZ | Kesi inaendelea |
| **7.** | Standard Chatered Bank (Hong Kong) Ltd (ICSID Case No. ARB/15/41) | | Mkataba wa Uwekezaji kati ya IPTL na TZ | TZ iliamuriwa kuilipa SCB-HK dola za Marekani milioni 185.45 (sawa na Sh. bilioni 432.7) pamoja na riba ya 2% kila baada ya miezi 6 kuanzia Septemba 1, 2018 |
| **8.** | Standard Chartered Bank (Hong Kong) Ltd[22] (ICSID Case No. ARB/10/20) | | Mkataba wa uwekezaji kati ya TANESCO na IPTL | TANESCO iliamuriwa kuilipa SCB–HK dola milioni 148.4 (sawa na bilioni 346) na riba ya 2% kila baada ya miezi 3 kuanzia Septemba 30, 2015 |
| **9.** | Standard Chartered Bank (ICSID Case No. ARB/10/12) | Fidia ya dola za Marekani milioni 118.6, pamoja na gharama za kesi, hasara & riba. | MIUMBI kati ya Uingereza na TZ | Mahakama ilitupilia mbali maombi ya SCB. Hata hivyo, baadaye benki ya SCB ilifungua mashitaka mawili tofauti kupitia tawi lake la Hong Kong na kushinda kama ilivyoonyeshwa ktk na. 7 & 8. |
| **10.** | Biwater Gauff (Tanzania) Ltd. (ICSID Case No. ARB/05/22) | Dola za Marekani milioni 20.2 | MIUMBI kati ya Uingereza na TZ | Mahakama iliikuta TZ na hatia ya kukiuka mkataba wa MIUMBI lakini hata hivyo haikutoa fidia ya fedha kwa Biwater Gauff (Tanzania) Ltd. |

Chanzo: Tovuti ya Benki ya Dunia https://icsid.worldbank.org/cases/case-database

Jedwali hapo juu linaonyesha kesi 10 zilizofunguliwa na wawekezaji dhidi ya Tanzania katika kituo cha ICSID kati ya mwaka 2005 na 2021. Kati ya kesi hizo 10, kesi 8 zilitumia MIUMBI kama nyenzo ya kuanzisha mashitaka dhidi ya Tanzania. Katika kipindi hicho, Tanzania ilifungua kesi moja tu dhidi ya wawekezaji, ambayo ni ICSID Case No. ARB/98/8, iliyofunguliwa na Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) dhidi ya kampuni ya IPTL mwaka 1998. Madai ya TANESCO kwa IPTL yalihusu IPTL kukiuka mkataba wake na TANESCO ambapo, katika hukumu yake, mahakama iliitaka IPTL kutekeleza mkataba huo. Hakukuwa na fidia yoyote ya kifedha iliyolipwa kwa TANESCO katika kesi husika.

## Hitimisho

Sura hii imeainisha MIUMBI iliyoingiwa na Tanzania na kuonyesha athari zake kwa nchi yetu. Athari kuu ni kuwa MIUMBI huibana Tanzania na kukandamiza haki yake ya kujiamulia mambo yake yenyewe. Kwa maana nyingine, nchi ya Kusini inaposaini MIUMBI inapoteza uwezo wa kutunga sera na sheria za kulinda uchumi na rasilimali zake kwa manufaa ya wananchi wake. Matokeo yake ni kuwa sera zinazotungwa ni zile zinazoongeza umaskini kwa wananchi huku zikinufaisha wageni.

Pale ambapo nchi ya Kusini hujaribu kuchukua hatua za kulinda rasilimali zake na kuratibu uwekezaji, wawekezaji huifungulia nchi hiyo mashitaka katika mahakama za

kimataifa ambazo zimeundwa mahususi kwa ajili ya kulinda maslahi ya wawekezaji. Kuna gharama kubwa sana katika uendeshaji wa kesi hizi nje ya nchi, ambazo ni mzigo kwa walipa kodi. Pia, adhabu inayotolewa ni kubwa sana kiasi cha kuifanya nchi ikope ili iweze kulipa fidia kwa wawekezaji.

Watetezi wa MIUMBI husema kuwa inasaidia kuvutia wawekezaji lakini dhana hii siyo sahihi. Kwanza, ukitazama orodha ya nchi zinazoongoza kwa uwekezaji nchini Tanzania, utaziona nchi pia ambazo hazina MIUMBI na Tanzania, kama India, Kenya na Umoja wa Falme za Kiarabu. Hii inamaanisha kuwa MIUMBI sio kigezo kikuu cha kuvutia uwekezaji. Ipo mifano mingi ya nchi za Kusini ambazo zimeamua kujiondoa katika MIUMBI na bado zinaendelea kupokea uwekezaji mkubwa tu kutoka nje ya nchi. Utafiti uliofanywa na shirika la *Public Citizen*[22] linalojihusisha na uangalizi wa biashara za kimataifa umeonyesha matokeo haya:

(i) Kati ya mwaka 2008 hadi 2017, nchi ya Ecuador ilisitisha MIUMBI ishirini na sita (26) na pia ilijiondoa kwenye mkataba wa ICSID mwaka 2009. Takwimu zinaonyesha kuwa uwekezaji kutoka ughaibuni uliongezeka kufikia dola za Marekani bilioni 17 mwaka 2018 kutoka dola za Marekani bilioni 13 mwaka 2008.

[22]*Public Citizen,* "Termination of Bilateral Investment Treaties Has Not Negatively Affected Countries' Foreign Direct Investment Inflows," Aprili 16, 2018. Imepatikana Juni 27, 2022 kutoka https://www.citizen.org/article/termination-of-bilateral-investment-treaties-has-not-negatively-affected-countries-foreign-direct-investment-inflows/

(ii) Nchi ya Bolivia ilijiondoa katika MIUMBI kumi na saba (17) kati ya mwaka 2009 hadi 2018 na katika kipindi hicho uwekezaji kutoka ughaibuni ulikua kutoka dola za Marekani bilioni 7.3 mwaka 2009 hadi dola za Marekani bilioni 11.8 mwaka 2018.

(iii) Mwaka 2010, nchi ya Afrika Kusini ilijiondoa katika miumbi 20 lakini bado uwekezaji kutoka ughaibuni ulizidi kuongezeka. Hata pale Afrika Kusini ilipositisha mkataba wake wa MIUMBI na Ujerumani mwaka 2014 bado uwekezaji kutoka Ujerumani kwenda Afrika Kusini ulizidi kuongezeka.

(iv) Mwaka 2014, nchi ya Indonesia ilitoa notisi ya kujiondoa kwenye MIUMBI 67 na mwaka 2016 India ilitoa notisi ya kujiondoa kwenye MIUMBI 58. Licha ya hatua hizo, uwekezaji kutoka ughaibuni umeendelea kuongezeka katika nchi hizo.

Kutokana na mifano hiyo, tunatoa mapendekezo yafuatayo:
(i) Tanzania ijiondoe kwenye MIUMBI yote.
(ii) Tanzania ijiondoe kwenye vyombo vya kimataifa vya utatuzi wa migogoro ya uwekezaji kama ICSID.
(iii) Sheria za ndani zinazotoa mwanya kwa wawekezaji kuiburuza Tanzania kwenye mahakama za kimataifa zifanyiwe marekebisho ili kuziba mwanya huo.
(iv) Mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ndani ya nchi iimarishwe kwa maslahi mapana ya utoaji haki kwa wote.

Tunapendekeza, pia, Katiba yetu ifanyiwe marekebisho ili kuweka kifungu kinacholinda uhuru na mamlaka ya mwisho ya dola la Tanzania juu ya utajiri asilia na rasilimali za Tanzania pamoja kulinda mifumo ya utoaji haki ya ndani ya nchi. Kwa kufanya hivyo Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza. Kifungu namba 366 cha Katiba ya Bolivia ya 2009 kinazitaka kampuni zote za kigeni zinazofanya kazi kwenye sekta za mafuta na gesi kuwa chini ya mamlaka ya dola la Bolivia na kinazuia migogoro kuamuliwa na mahakama za nje. Hali kadhalika, katiba ya Ecuador ya mwaka 2008 ina kifungu (namba 422) kinacholinda mamlaka ya mwisho ya dola la Ecuador kufanya maamuzi ya kisheria na pia kinapiga marufuku kusalimisha mamlaka hayo kwa mikataba au vyombo vya kimataifa[23]. Licha ya vifungu hicho, uwekezaji wa kigeni haukupungua katika nchi za Bolivia na Ecuador. Kwa kudhibiti kampuni za wawekezaji, nchi hizo ziliweza kufaidika na utajiri asilia na rasilimali zake ambazo zilitumiwa kuboresha ustawi wa wananchi wake.

Ni vema pia vyombo vyetu vya utoaji haki viwe mstari wa mbele katika kulinda mamlaka ya ndani ya utatuzi wa migogoro. Mahakama kuu ya Ajentina, kwa mfano, ilitamka katika hukumu ya Jose Cartellone Construcciones Civiles S.A. dhidi ya Hidroelectrica Norpatagonica S.A. ya mwaka 2004 kuwa mahakama ndiyo mlinzi mkuu wa katiba na kamwe haitaruhusu mamlaka hayo kuporwa na chombo

[23]Katia Fach Gomez, "Latin America and ICSID: David versus Goliath," *Law & Business Review of the Americas* 17, No. 2 (2011), uk. 203.

chochote cha kimataifa, na kwa mantiki hiyo, mahakama kuu ya Ajentina inayo mamlaka ya kupitia upya mashauri yote yaliyoamuliwa na vyombo vya kimataifa hata pale ambapo pande mbili zinakuwa zimekubali kuondoa haki yao ya kukata rufaa.

Kitabu hiki kimeandikwa mahususi ili kitumike kama nyenzo ya kujielimisha kuhusu mikataba ya uwekezaji kati ya nchi mbili (MIUMBI). Kama ilivyofafanuliwa ndani ya kitabu hiki, MIUMBI ni mikataba inayosainiwa kati ya nchi mbili kwa lengo la kulinda na kuhamasisha uwekezaji unaofanywa na nchi mojawapo katika nchi ya pili. Mikataba hii imekuwa ikipigiwa chapuo na nchi za Magharibi, mashirika ya kimataifa kama Benki ya Dunia, Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF) na Shirika la Kimataifa la Biashara (WTO) kama njia pekee ya kuvutia uwekezaji katika nchi maskini na hivyo kupelekea kukua kwa uchumi na kupungua kwa umaskini katika nchi hizo. Hata hivyo, nchi zinazopokea uwekezaji zimekuwa zikilalamika kuwa MIUMBI imekuwa ikitumika kama nyenzo za kuendeleza unyonyaji na uporaji wa rasilimali za nchi maskini unaofanywa na nchi tajiri. Kwa kuwa nchi yetu, Tanzania, ni miongoni mwa nchi zilizosaini MIUMBI, basi itakuwa ni jambo jema kwa wananchi wote, wakiwemo watunga sera, kujielimisha kuhusu chimbuko na asili ya mikataba hii, athari zake kwa nchi yetu na jinsi ya kujinasua.